MID WEEK JACKPOT!
TZS. 553,549,430
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**CAG** aona shida katika tozo mizani TANROADS

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Aprili 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581283
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Utafiti wabaini njia 3 kujikinga VVU

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa pamoja na Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Alhad Omar wakati wa futari Ikulu jijini Dar es Salaam juzi.
**PICHA: IKULU**

## Majaliwa ataka viongozi wa dini kusimamia haki, amani

UKURASA 2



## Mwinyi: Lipeni wafanyakazi mishahara mapema maandalizi Eid

UKURASA 2

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**COMMERCIAL CASE NO 118 OF 2022**

**EQUITY BANK (T) LTD.............................................................................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**REGIONAL LOGISTICS LTD..............................................................1ST DEFENDANT**
**CATHERINE KETTIE MHANGO.........................................................2ND DEFENDANT**
**PETER ODONGO KITIWA...................................................................3RD DEFENDANT**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**To:**
**1.MANAGING DIRECTOR,**
**RGIONAL LOGISTICS LTD,**
**P.O.BOX 75705,**
**DAR ES SALAAM.**

**2.CATHERINE KETTIE MHANGO,**
**P.O.BOX 75705,**
**DAR ES SALAAM.**

**3.PETER ODONGO KITIWA,**
**P.O.BOX 75705,**
**DAR ES SALAAM.**

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set in the plaint service of the summons in you has ordered by means of publication. You are directed to collect copies of the case documents from the court's Registry, P.O. Box 12533, Dar es salaam. You are hereby summoned to appear in this court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on **3th May 2023 at 09:00am before Hon. A.MBAGWA,Judge** for **Orders. TAKE FURTHER NOTICE THAT** should you default to enter appearance as herein provided, the matter will proceed and decision may be given in your absence.
**Given under my hand and Seal of the Court this 5th day of April 2023.**

**DEPUTY REGISTRAR**
**COMMERCIAL DIVISION**
**DAR ES SALAAM**

# Utafiti wabaini njia 3 kujikinga VVU

**Na Restuta James**

UTAFITI wa kitabibu umeongeza matumaini katika vita dhidi ya Virusi vinavyosababisha ugonjwa wa Ukimwi (VVU), baada ya kuja na dawa kinga zinazoweza kumkinga mtu asiambukizwe virusi hivyo.

Wataalamu wa afya wametaja dawa kinga hizo kuwa ni pete kinga inayowekwa ukeni na nyingine ni dawa ya sindano anayochomwa mtu kumkinga ndani ya miezi miwili.

Akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu taasisi isiyo ya kiserikali ya DARE Tanzania, Dk. Lilian Mwakyosi, alisema pete kinga ni miongoni mwa njia salama na rahisi kutumia ili kujikinga na VVU hususani kwa wasichana na wanawake.

Alisema pete hiyo inayojulikana kwa jina la kitaalamu 'Dapivirine Vaginal Ring (DVR)', imewekewa dawa maalumu ya kuzuia maambukizi ya VVU, yanayoweza kumpata mwanamke wakati wa kujamiiana.

Alisema DVR ni kinga mahsusi kwa wanawake kwa kuwa inawapa uhuru wa kuamua kujikinga bila kuhitaji ruhusa ya mwenza, kwa kuwa wakati wa kujamiiana mwanmume hawezi kuhisi utofauti.

"Hii ni miongoni mwa njia ya kukabiliana na VVU iliyoidhinishwa hivi karibuni na Shirika la Afya Duniani (WHO), ikijumuisha pete ya ukeni, vidonge na sindano. Njia hizi zinakuja kuziba pengo lililokuwapo katika kujikinga...wote tunahitaji kujikinga, lakini tuna mahitaji tofauti," alisema Dk. Lilian.

Kadhalika, alisema njia hizo zinakwenda sambamba na nyingine zilizokuwapo awali ikiwamo kuepuka ngono zembe, kutumia kondomu na dawa za kufubaza VVU kwa wale ambao wameshabainika kupata maambukizi.

Alisema sindano, vidonge na pete ya ukeni ni matokeo ya utafiti wa kitabibu unaoendelea duniani, katika kukabiliana na VVU.

Vile vile, pete hiyo ina dawa ambayo inaweza kukabiliana na VVU ndani ya siku 28 na mtumiaji anapaswa kuitoa na kuweka nyingine baada ya siku hizo ikiwa atahitaji kufanya hivyo.

"Hii ni njia inayoongezeka ili kukabiliana na VVU na itasaidia sana wanawake ambao hawawezi kutumia njia zilizopo sasa ambazo nyingine zinahitaji maamuzi ya mwenza. Inaongeza nguvu kwa mwanamke kuweza kuwa na uchaguzi wa kujilinda," alisema.

Alisema utafiti zaidi unaendelea kufanyika duniani ili kupata tiba kamili ya ugonjwa huo na kuwasihi Watanzania kuendelea kujikinga na kutumia dawa zilizopo ili kuepuka maambukizi.

Mratibu wa Asasi ya COMPASS nchini, Francis Luwole, alisema sindano inamchanganyiko wa dawa mbili zinazodhibiti kuzaliana kwa VVU pale vinapoingia kwenye mwili ambao umetumia dawa hiyo.

Alisema tofauti na pete, sindano inakaa mwilini kwa miezi miwili na kwamba baada ya muda huo, mtumiaji anaweza kuchoma tena ili kujikinga.

Hata hivyo, alisisitiza kwamba dawa hiyo haimzuii mtu kuendelea kujilinda kwa kuacha ngono zembe na hazizuii magonjwa mengine ya zinaa.

"Siku hizi utakuta vijana wanatembea na dawa za kuzuia mimba sio kondomu...hili ni jambo la hatari na inatuthibitishia kwamba elimu zaidi inahitajika kutolewa ili vijana waweze kujikinga dhidi ya VVU na magonjwa mengine ya zinaa," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mratibu wa masuala ya Ukimwi katika Manispaa ya Kinondoni, Dk. Amos Kitonga, alisema takwimu zinaonyesha kwamba asilimia 95 ya Watanzania wamepima VVU na asilimia 98 ya waliobainika kuwa na maambukizi wanatumia ARV.

Alifafanua kuwa vifaa vya kupimia VVU vinapatikana nchi nzima kuanzia zahanati, ikiwa ni mpango wa serikali kurahisisha upimaji na ushauri nasaha kwa wananchi.

Mtendaji Mkuu wa asasi isiyo ya kiserikali Mulika Tanzania, Hussein Melele, alisema vyombo vya habari vina nafasi ya pekee ya kuendelea kuhabarisha umma kuhusu VVU na UKIMWI kwa kuwa Tanzania ina idadi kubwa ya vijana.

Hata hivyo, alisema dawa kinga hizo bado hazijaidhinishwa kutumika nchini. Kwa Afrika, zimeidhinishwa Kenya, Uganda, Rwanda, Zimbabwe na Afrika Kusini, ambako zimeanza kutumika.

# Majaliwa ataka viongozi dini kusimamia haki, amani

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani) amewataka viongozi wa dini nchini kusimamia haki, kuienzi na kusimamia amani kwa manufaa ya wananchi wa sasa na vizazi vijavyo.

"Niwasihi sana ninyi viongozi wetu wa dini kutukumbusha mara kwa mara sisi, waumini na watu wote kuhusu umuhimu wa kusimamia haki na kudumisha amani na kuiombea nchi yetu na viongozi wake," alisema Majaliwa.

Alisema hayo jana katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, wakati wa ibada ya harambee ya ujenzi wa shule ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki Ziwa Victoria-Mwanza, iliyofanyika katika Kanisa la KKKT Imani wilayani Ilemela, mkoani Mwanza.

Kupitia harambee hiyo, kanisa hilo limefanikiwa kukusanya Sh. 119,563,000 zikiwamo fedha taslimu, ahadi na vifaa.

Waziri Mkuu amewataka viongozi wa dini nchini kutochoka kufundisha na kulea vijana katika maadili mema na kuthamini kufanya kazi halali.

"Katika nyakati hizi ni ukweli ulio wazi kuwa kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii yetu," alisema Majaliwa kupitia hotuba yake.

Alisema, alisema kushuka kwa maadili ni jambo lenye athari mbaya kwa jamii na taifa kwa ujumla hali inayochangia kurudisha nyuma juhudi za kujiletea maendeleo na kuifanya kazi ya kuondoa umaskini kuwa ngumu.

Anaamini kuwa viongozi wa serikali, dini na vyama vya siasa wakishika mafundisho ya dini na kuwa na hofu ya Mungu, maovu mengi yatapungua na nchi kuongozwa vizuri.

Alisisitizia suala la elimu na umuhimu wake kwa maendeleo ya taifa lolote na kutaka viongozi wa dini kusaidia kuzungumza na wazazi.

Amelipongeza Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki ya Ziwa Victoria-Mwanza na waumini kwa ujumla kwa kujitoa kwa hali na mali kwa kufanya kazi ya Mungu kwa kuhakikisha jengo linakamilikia hasa ikizingatiwa fedha zote ni michango ya waumini na kubainisha kuwa, kitendo kilichofanyika ni chema na kinaleta baraka zote.



Awali, Askofu Mkuu wa KKKT Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria-Mwanza, Andrew Petro Gulle, alisema ujenzi wa shule ya kanisa hilo unakadiriwa kuwa Sh. 2,350,000,000 na mpaka sasa Sh. 430,000,000 zimetumika kujenga boma la madarasa 10 na jengo la utawala.

Waziri Mkuu alichangia Shilingi milioni tano zitakazotumika kukamilisha kazi ya ujenzi wa shule Dk. Mabula alichangia Shilingi milioni mbili.

# Mwinyi: Lipeni wafanyakazi mishahara mapema maandalizi Eid El Fitr

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi ameagiza malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa serikali kufanyika mapema kwa ajili ya matayarisho ya Sikukuu ya Eid El Fitr.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilieleza kuwa Rais Mwinyi ameagiza malipo hayo yaanze kufanyika Aprili 14, mwaka huu.

Kwa mujibu wa tamko la Rais, hatua hiyo inalenga kuwapa muda wa kutosha wafanyakazi wa serikali kufanya maandalizi ya sherehe hizo.

Sherehe hizo zinatarajiwa kuangukia kati ya Aprili 21 au 22 kutokana na kuandama kwa mwezi na kuashiria mwisho wa mwezi.

Sehemu ya taarifa hiyo pia ilieleza: "Pia Rais Mwinyi amewashukuru wafanyakazi wa serikali kwa ushirikiano wao wakati wote wa ibada tangu kuandama kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan".

VIJANA NA QURAN

Wakati huo huo, Dk. Mwinyi akiwa katika hafla ya kilele cha tuzo za kimataifa za Quran tukufu zilizofanyika jana, jijini Dar es Salaam alisema tuzo za kimataifa za Quran tukufu ni fursa ya kuvitangaza vipaji vya vijana kimataifa na kuwapa nafasi ya kuonekana na kufika mbali zaidi.

Dk. Mwinyi alisema utaratibu huo, utasaidia jitihada za kuimarisha maadili mema kwa kuwalea vyema vijana kiroho na kitabia.

"Hapana shaka sote tunatambua kuwa dunia inakabiliana na changamoto nyingi zikiwamo jitihada za kupenyeza harakati za kuharibu maadili. Kwa bahati mbaya jitihada hizi zimepata uungwaji mkono hata na baadhi ya Watanzania," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema lazima kuwapo na mikakati imara na mbinu madhubuti za kuyalinda maadili mema katika kizazi cha sasa na vijavyo.

Kadhalika, Dk. Mwinyi alisema ni vyema kuwahimiza vijana kuzidi kushikamana na Quran kwa kuisoma, kuihifadhi na kuyafuata maamrisho na makatazo yake, kwasababu kitabu hicho ndio muongozo kwa wanadamu wote.

Aidha, Dk. Mwinyi alipongeza jumuiya ya kuhifadhisha Quran Tanzania chini ya Shekhe Othman Kaporo, kwa kuwa mfano mwema kwa taasisi nyingine na shule za ngazi mbalimbali zinazofundisha, kulea na kutoa wataalamu mahiri wenye maadili bora.

"Leo katika ukumbi huu tumeshuhudia vijana wa kitanzania waliohifadhi Quran tukufu, huku wakiwa na fani tofauti. Hali hii inatokana na juhudi kubwa zinazofanywa kwa takriban miaka 31 na Shekhe Kaporo na timu yake katika kuhifadhisha Quran," alisema.

Aliwapongeza washindi wa tuzo mbalimbali ambazo alisema zitawaongezea hamasa washiriki na kuzidi kuitumikia Quran na kuendelea kuwa chachu ya maadili mema katika jamii.

Kupitia mkusanyiko huo Dk Mwinyi aliwataka wananchi kuendelea kuwaombea viongozi wao akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake kwa sababu wanafanyakazi kubwa katika kuendelea kudumisha amani ya nchi, kuimarisha ustawi na uchumi pamoja na kuleta maridhiano.

"Kazi hii ina changamoto kubwa, naomba muendelee kumuombea yeye pamoja na kutuombea sote tunaomsaidia katika kazi hii kubwa," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (kushoto), akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Goodluck Mlinga kwaajili ya kuukimbiza wilayani humo jana. Wa (pili kulia), ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge kitaifa, Abdalla Shaib Kaim. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CAG aona shida katika tozo mizani TANROADS

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini makosa katika utozaji wa faini za kuzidisha uzito wa mizigo kwenye mizani zinazomilikiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) kwa mwaka 2021/22, CAG Charles anasema kuwa baada ya kufanya mapitio ya faini za kuzidisha uzito wa upakiaji mizigo zilizotozwa na TANROADS katika mizani 13 kwa mwaka wa fedha 2021/22, amebaini magari 11,594 yalitozwa faini pungufu ya kiasi kilichotakiwa kutozwa, kwa jumla ya Dola za Marekani 466,449.

Pia, magari 134 yalitozwa faini zaidi ya kiwango kilichotakiwa, kwa jumla ya Dola za Marekani 10,958, kinyume cha aya ya 11 ya jedwali namba tatu la udhibiti wa uzito wa magari wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

CAG anatoa angalizo kuwa, utozaji wa faini kinyume cha taratibu unaweza kusababisha upotevu wa mapato na athari za kisheria kwa kutofuata kanuni, jambo ambalo linaweza kuharibu sifa na hadhi yake.

Kuhusu miamala isiyosuluhishwa kwenye taarifa za mifumo ya ankara na mfumo wa GePG (Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroniki), CAG anasema katika miamala 682, tofauti iliyobainika ni ankara zenye viwango vilivyolipwa kwa ziada (overpaid) kwenye mfumo wa Data Bridge.

Kutokana na makosa hayo, CAG anapendekeza TANROADS ifanye mapitio na kusahihisha kanuni ya mfumo inayokokotoa uzito wa ekseli na uzito wa magari ili kuhakikisha utozaji viwango sahihi vya faini za uzidishaji uzito, kwa mujibu wa udhibiti wa uzito wa magari wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kuhusu kutokuwianisha kwa mifumo ya TANROADS, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anasema amebaini mambo kadhaa yanayohusu uwianishaji wa mifumo tumizi kwa wakala huo.

CAG anabainisha kuwa TANROADS inatumia mifumo mitatu tofauti ya mizani, ambayo ni Data Bridge, Smart Scale na Tload, kwa madhumuni sawa ya upimaji.

Amebaini pia ni mizani 13 pekee kati ya 63 imeunganishwa kwenye seva kuu, akisisitiza hali hiyo inaleta hatari ya udanganyifu kutokana na ufuatiliaji usiotosheleza.

Amependekeza TANROADS ifuate miongozo ya usanifu wa kiutendaji na kuhakikisha programu zote za mizani zinazojitegemea zimeunganishwa kwenye seva kuu kwa ufuatiliaji unaofaa.

**DOSARI HESLB**

CAG pia anasema amebaini upungufu katika Mfumo Fungamanishi wa Mikopo (ILMIS) wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Amesema katika mapitio ya mfumo fungamanishi wa usimamizi wa mikopo, amebaini upungufu katika udhibiti wa uhakiki wa malipo ya marejesho ya mikopo ya HESLB.

Amesema kukosekana kwa udhibiti wa kutosha wa uingizaji taarifa za marejesho ya mikopo, unaweza kusababisha kurekodiwa kwa marejesho yasiyokuwa na nambari za risiti za malipo katika mfumo.

Hiyo inatokana na ukosefu wa udhibiti wa uhakiki wa kutosha katika mchakato wa kuingiza malipo.

Pia, CAG anasema kuingiza malipo bila nambari ya risiti, kunaweza kusababisha kurekodiwa kwa malipo yasiyolipwa katika mfumo; hatimaye kusababisha taarifa isiyo sahihi ya bakaa ya mkopo, na kusababisha athari katika mchakato wa malipo ya mkopo.

Amependekeza HESLB ifanye mapitio na kuimarisha udhibiti wa mfumo katika mchakato wa uhakiki wa malipo ya marejesho ya mkopo ili kuhakikisha kuwa mfumo unathibitisha taarifa zinazoingizwa na kuzuia kuingiza malipo bila nambari ya risiti.

Vilevile, anasema mapitio ya mfumo fungamanishi wa usimamizi wa mikopo, yalibaini upungufu katika udhibiti wa uhakiki wa malipo ya marejesho ya mikopo ya HESLB.

Ameonya kuwa hali hiyo ina uwezekano wa kusababisha marejesho yasiyolipwa katika mfumo, ambayo yanaweza kusababisha taarifa isiyo sahihi ya bakaa ya mkopo na kusababisha athari katika mchakato wa malipo ya mkopo.

# Wadau: Kuna upotoshaji ununuzi Tanga cement

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa biashara nchini wameibuka na kudai kuna baadhi ya watu wanaopotosha umma mpango wa kampuni ya Twiga cement kuinunua Tanga cement kwa nia ya kutaka kuzuia mchakato huo.

Mchakato huo unadaiwa kupingwa katika sekta ya saruji, na kupotosha ukweli na kutengeneza taarifa tofauti.

Chanzo cha kuaminika cha taarifa hii kimedai hivi karibuni baadhi ya watu kujaribu kutatiza mchakato huo wa muamala na kwamba kuuzuia mpango huo kunaweza kusababisha hasara ya uwekezaji.

"Taarifa za hivi karibuni zinapendekeza kwamba shughuli inayopendekezwa itakiuka sheria ya ushindani wa haki, kwa kuvuka kiwango cha juu cha kutawala soko kwa pamoja cha asilimia 35 na kutaja bei ya manunuzi ya Sh. bilioni 137, kauli hizi si sahihi na zina lengo la kupotosha wadau na umma wa Tanzania," kilidai chanzo hicho.

Aidha, Desemba 2022, Scancem International ilituma maombi kwa Tume ya Ushindani (FCC) kwa mara ya pili, kwa nia ya kupata asilimia 68.33 ya mtaji wa hisa wa Tanga Cement.

Chanzo hicho kilibainisha kuwa ombi hilo jipya liliwasilishwa kulingana na hali ya soko lililokuwapo mwaka 2022 na liliidhinishwa bila masharti na FCC Februari mwaka huu, kwa kuwa sehemu ya soko iliyojumuishwa iko chini ya kiwango cha kisheria cha asilimia 35 na inathibitisha kuwa hakuna kutawala soko.

Kimefafanua kuwa uamuzi huo wa FCC haukupingwa na Baraza la Usuluhishi la Ushindani (FCT) na baraza hilo halijatoa uamuzi kulingana na uamuzi huo.

"Sekta ya saruji nchini ina sifa ya kuzidiwa kwa uzalishaji tangu kuwasili kwa Dangote na Huaxin. Zaidi ya hayo, mwaka huu, angalau wazalishaji wengine watatu wa saruji wanaongeza karibu asilimia 15 ya uwezo wa ziada wa saruji.

Kilieleza kuwa sera ya saruji duniani kote, kama Scancem International ni kuongeza ufanisi na utendaji wa uzalishaji ili kupunguza gharama ya uzalishaji na kuwa na ushindani sokoni, kwa bei ya chini.

Kilisema hiyo ni kanuni ya kiuchumi inayokubalika kwa jumla ya ugavi na mahitaji, na kwamba ugavi mkubwa, bei ya chini, muamala huo utahitaji uwekezaji wa ziada mara tu utakapokamilika, kwa kuwa utendaji wa kiufundi wa Tanga Cement lazima uimarishwe.

Hata hivyo kilisema 2021 Twiga Cement ililipa zaidi ya Sh. bilioni 80 katika kodi, mrabaha, na ushuru mbalimbali, huku Tanga Cement ikiendelea kupata hasara, kama inavyothibitishwa katika notisi yao kwa wanahisa ya Machi 24, mwaka huu.

"Kuanzia 2016 hadi 2021, Tanga Cement imepata hasara ya jumla ya zaidi ya Sh. bilion 43, na kuwa mbaya zaidi mwaka 2022, kumaanisha kwamba hakuna kodi ya mapato inayolipwa," kilisema.





Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (watatu kulia), akikabidhi funguo ya gari kwa mshindi wa kampeni ya Benki ni SimBanking, Mayani Yahaya Hassan, mkazi wa Dodoma, baada ya kuibuka kidedea katika droo iliyochezwa mapema mwezi huu, katika hafla iliyofanyika wilayani humo mwishoni mwa wiki. Wengine ni wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi Tarime wafurahia alama za mipaka rasmi kuwekwa SENAPA

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

WANANCHI wa kata tatu katika vijiji saba wilayani Tarime, mkoani Mara, wameridhia uwekwaji wa alama za mipaka katika Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENAPA), huku wakiomba serikali kuwapatia huduma ya maji baada ya Mto Mara kuwa ndani ya hifadhi.

Wakizungumza jana wakati wa uwekaji alama za mwisho katika Kijiji cha Nyabilongo, Kata ya Kwehancha upande wa Tarime, walisema hawana pingamizi na uhifadhi na wamekubali alama hizo ziwekwe wataziheshimu, lakini ni muhimu wakapatiwa maji kwa ajili ya mifugo na binadamu.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyabilongo, Simion Chacha alisema: "Mahusiano na SENAPA ni mazuri tunafanya vikao mara kwa mara hadi imefikia kwamba shughuli za uwindaji wanyamapori hazipo, lakini nikienda kijijini wananchi wananiuliza maji ya Mto Mara tunafanyeje?"

"Kwa mazungumzo na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), waliahidi kuchimba mabwawa ambayo hadi sasa bado, tunawaomba waharakishe ili tupate maji ya mifugo na binadamu, maji ni uhai, maji ni maisha yetu," alisema.

Aidha, alisema mpaka uliopita kwa mujibu wa tangazo la serikali ni sahihi hawana malalamiko kwasababu walishirikishwa kikamilifu kwenye kila hatua.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyabilongo, Michael Mseti alisema haki imetendeka na hadi sasa hakuna mwananchi aliyelalamika, awali ilikuwa changamoto kwasababu wananchi walifanya shughuli zao kwa kutojua mpaka ulipo.

"Kwa kuwapo mpaka sasa amani itaendelea kudumu, kijiji hiki ni moja ya vyenye uhusiano mzuri na hifadhi na katika Shule ya Msingi Nyabilongo tunaendelea na ujenzi wa nyumba za walimu kwa fedha zaidi ya Sh. milioni 107 kutoka SENAPA. Nawaomba wananchi wazilinde," alisema.

Aliiomba SENAPA kuwapatia wananchi chanzo kipya cha maji baada ya Mto Mara kwa kunywesha mifugo na matumizi mengine, ikishakuwa ndani ya hifadhi hawataweza ni muhimu wakapewa huduma hiyo.

Mwananchi wa kijiji hicho, Mnuko Chacha, alisema: "Maji ni chakula cha wananchi na mifugo, kwasababu tumeambiwa tuheshimu mipaka tunajiuliza bila kuwekewa maji mengine ya kunywesha na kutumia itakuwaje, Tunaomba watuharakishie malambo ili kuondokana na tatizo la maji."

Naye, Gatti Gichogo alisema: "Uwekaji alama umeenda vizuri, lakini changamoto kubwa ni maji, hatuna sehemu ya kunyweshea mifugo, kina mama hatuna sehemu ya kuchota maji, tulikuwa tunategemea sana Mto Mara, naomba sana mshughulikie."

Mwenzeshaji Jamii wa Kijiji cha Nyabilongo, Marwa Meng'anya alishukuru SENAPA kwa hatua hiyo na walikuwa wanakutana na maswali mengi kwenye mikutano ya hadhara na kwamba kwa mipaka kujulikana kutaondoa migogoro.

Ofisa Mpima wa Wizara ya Ardhi, John Solo alisema uhakiki na kusimika vigingi kumekwenda vizuri kutokana na mwitikio wa wananchi walioelimishwa umuhimu wa kuwa na mipaka inayoonekana ambayo iliwekwa kisheria tangu mwaka 1968.

Alisema kulikuwa na changamoto ya mvua na uelewa lakini walipata ushirikiano kwa wenyeviti wa vitongoji, vijiji, watendaji wa kata na wananchi kwa ujumla

Mrasimu Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Salum Mzuzuri, alisema kazi yake kubwa ilikuwa ni kutafsiri GN (tangazo la serikali) 235 ya mwaka 1968 katika kipande cha kilomita 29 kuanzia mpaka wa Tanzania na Kenya.

Alisema eneo hilo linahusisha safu za milima, eneo oevu, Mto Swetu na Mto Mara na kwamba walikuwa wanapima na kuwapa uelewa na kama kuna changamoto wawasiliane na serikali kutatua kuliko kuharibu alama.

"Katika kutafsiri tulibaini kuna maeneo wananchi wameingia eneo la hifadhi kwa umbali mrefu kutokana na kwamba hakukua na alama, sasa tumeongeza alama umbali wa mita 50 hadi 200 ili waone.," alisema na kuongeza:

"Awali kuna ambao waligoma kiasi cha kukataa hata kufanya vibarua, lakini kadiri tulivyoendelea na kuwaelimisha walikubali, leo wamejitokeza wengi sana wanaomba vibarua, lakini tumechukua wachache." Mzururi alisema faida ya mipaka kutambuliwa ni kuendeleza ujirani mwema, kuwekeza na kupata mapato pamoja ana ajira kwenye hifadhi.

Ofisa Mpima Ardhi wa Mkoa wa Mara, Pastory Katanga, alisema walianza kazi hiyo Machi 27, mwaka huu, na kwamba kero ya kutambua mipaka ni ya zaidi ya miaka 30. "Ni mgogoro umetusumbua hatukupata dawa, lakini leo tumepumua sasa kero imekwisha na sasa ni kujenga uhusiano mwema na SENAPA kwa maendeleo yetu sote," alisema.

TATEPA
TATEPA LIMITED

**NOTICE OF ANNUAL GENERAL MEETING**

Notice is hereby given that the 29th Annual General Meeting of the Company in respect of the year ended 30th September 2022 will be held at Coral Beach Hotel Resort, Off Chole Lane, Yacht Club Road, Msasani Peninsula Dar Es Salaam on Thursday of the 27th of April 2023 at 10:00 East Africa Time.

**AS ORDINARY BUSINESS**

1. Confirmation of the Minutes of the 28th Annual General meeting held on Thursday the 26th of May 2022 at the Hotel Slipway Conference Centre, Slipway Road, Msasani Peninsula Dar Es Salaam at 11:30 AM EAT.
2. To receive, consider and adopt the report of the Board of Directors, the Audited Financial Statements for the year ended 30th September 2022, and the report of the auditors' thereon.
3. To approve no payment of dividend for the year 2022 as recommended by the Board of Directors of the Company.
4. Appointment of Directors: The Directors were appointed for a period of two years in the last AGM and hence no appointments are due.
5. Any other business

A proxy form is attached in hereto and must be lodged at the registered office of the Company not less than 48 hours before the commencement of the meeting.

**BY ORDER OF THE BOARD**

Rozmin A Jafferali Secretary
Tatepa Public Limited Company
P.O BOX 700 Tukuyu-Mbeya, Tanzania
rozmin@tatepa.com

## Mshindi kampeni CRDB akabidhiwa Toyota Crown

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya CRDB imekabidhi gari aina ya Toyota Crown kwa mshindi wa kampeni ya "Benki Ni SimBanking" kwa mwezi Februari na Machi, Mayani Yahaya Hassan, mkazi wa Dodoma.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi zawadi kwa mshindi huyo iliyofanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma, Meneja wa Kanda ya Kati wa Benki ya CRDB, Chabu Mishwaro alisema, mshindi huyo alipatikana katika droo ya kwanza ya kampeni hiyo iliyofanyika Aprili 6, mwaka huu. "Mayani ni mmoja wa wateja ambao wamekuwa wakitumia SimBanking kufanya miamala yao ya kifedha, jambo ambalo lilimpelekea kuingia katika kinyang'anyiro cha ushindi, na kuibuka kidedea baada ya droo kuchezeshwa," alisema Chabu.

Alibainisha kuwa katika kusaidia jitihada za serikali za kuchochea uchumi wa kidijitali nchini, kampeni ya "Benki Ni SimBanking" imekuwa ikihamasisha wateja kufanya miamala kidijitali kupitia SimBanking na kuachana na matumizi ya fedha taslimu.

Alisema inafanyika kwa muda wa miezi 10 hadi Desemba mwaka huu, kila siku wateja wanajishindia zawadi, pia kuna zawadi za mwezi, miezi miwili na zawadi kubwa ya Toyota Vanguard ambayo itatolewa mwishoni wa kampeni.

Akikabidhi zawadi hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alipongeza Benki ya CRDB kwa kuandaa kampeni hiyo ambayo alisema sio tu inachochea matumizi ya mifumo ya kidijitali ya utoaji huduma, bali pia ujumuishi wa kifedha kwa wananchi.

Kimweri alisema serikali imekuwa ikitilia mkazo matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa wananchi ili kuendana na kasi ya maendeleo kote duniani na kuwasihi wateja na wananchi kutoa ushirikiano kwa Benki ya CRDB na kushiriki katika kampeni hiyo ya "Benki ni SimBanking".

Mshindi aliishukuru Benki ya CRDB kwa zawadi hiyo ya gari huku akibainisha siri ya ushindi ni kujenga utamaduni wa kutumia SimBanking kufanya miamala yake yote ya kifedha.

"Ninafurahia sana kufanya miamala kupitia SimBanking iliyoboreshwa, imekuwa rahisi na nafuu sana kutumia. Sasa hivi miamala yangu yote ninakamilisha kupitia SimBanking, iwe kufanya malipo kupitia CRDB Lipa Namba, kutuma pesa, kulipia bima, kulipia kodi na kutoa fedha kwa CRDB Wakala/ ATMs na Tawini bila ya kadi," alibainisha Mayani.

# TANGAZO

TEMBO NICKEL

## VACANCIES

### COMMUNITY RELATIONS MANAGER – NGARA (RE-ADVERTISED)

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit **Community Relations Manager** to join the Tembo Nickel Project Team. S/he will have full responsibility for the assigned activities and be one of the primary interfaces with the identified local stakeholders. S/he will maintain regular communications with local government officials and other strategic partners at Village, Ward, Districts and Regional level.

The successful candidate will report to the S**ite General Manager**
**Duty Station: Tembo Nickel Project Site- Ngara**
**Roster: 6/3**

**Duties and Responsibilities**
- Manage the daily operations of community relations, providing guidance, leadership, and direct support in all aspects of service provision.
- Ensure smooth and functional Community Relations programs maintaining efficient systems and ensuring delivery of quality services.
- Manage budgets and approve expenses for Community relations related costs, ensuring costs are maintained within allocated budgets.
- Provide mentorship and support to staff around professional development, workload management, trauma-informed approach, and staff wellness.
- Cultivate an environment of teamwork through regular Team meetings and on-going training.
- Cultivates collaborative relationships with varied community stakeholders.
- Coordinates closely with Communication Team and Government Relations colleagues to ensure consistent, appropriate communications and timely follow-up.
- Ensure that all community grievances are resolved following Tembo Nickel process and compliance to international standards.

**Qualifications and Competencies**
- Master's degree in Social, Economic, Environmental, International Development, Rural Planning, Public Administration and Policy or other relevant field or experience.
- 15 years of work experience in Community relations with 5 years in senior Management.
- Solid understanding of environmental and social risks and safeguards, International Standards and Human Rights.
- Ability to engage and enable active participation of regional administration, district local government authority and local communities.
- Ability to develop plans, budgets, and reports.
- Mining experience will be an added advantage.

### SAFETY SYSTEMS & COMPLIANCE SPECIALIST

**Position Summary:**
Safety System & Compliance Specialist provides general Safety system support and legal requirements compliance to the health and safety team and the site al large, including but not limited to Checking all the documents on the occupational health and safety management system and advice their review to the responsible document holder.

The successful candidate will report to the **Safety Lead**
**Duty Station: Ngara**
**Roster: 6/3**
**Duties and Responsibilities**
- Ensure administration and management of the health & safety management system in line to the ISO45001:2018.
- Identifying all legal requirements and Appointments pertaining to Mining act and OSHA act.
- Ensure compliance to applicable codes, legislation and procedures including health and safety.
- Interact and cooperate with all department members and ensuring support in filling and documenting work-related documents.
- Designing Health and safety auditing tool/audit system to ensure compliance.
- Communicate audit outcomes with the relevant heads of department and ensure actions are closed out in a timely manner.
- Identifying all elements of TNCL safety framework system establishing an audit system to ensure compliance and audit compliance to current or active permissions and licenses.
- Organize and maintain a document control system, team meetings, solve safety issues, coordinate audits, and inspections, track corrective actions and incident data, review important safety documents and other duties that require a high degree of attention to detail.
- Assist in to make improvement and implement required changes relation to health and safety management system.
- Manage the operation of the document control centre to ensure that all users have the latest version of appropriate documentation in a timely manner.
- Develop and maintain a comprehensive filling system and computer database/system for all documents to be retained in the documentation in a control centre.
- Ensure that department documents are well managed, organizing an archiving system, retrieving documents upon request, and outlining a long-term storage strategy.
- Ensure a timely, accurate and efficient preparation and management of documents, control the numbering, sorting, filing and retrieval of both electronic and hard copy documents produced by the departments.
- Maintain quality assurance of all outgoing documentation, track, transmit and accurately file hard copy and electronic documents.
- Coordinate multi-office and work-sharing information in a timely manner. Perform any other duties that may be required from time to time as directed by your supervisor / Manager.

**Qualifications**
- Diploma/Degree in OHS Management system.
- ISO 45001:2018 OHS Management system certification.
- Any Health and Safety related qualifications.
- 5-10 years' experience in a similar role.
- Any other relevant training certification to deliver role requirements.

### DOCUMENT CONTROLLER/SAFETY ADMINISTRATOR

**Position Summary:**
Safety Administrator provides general administration and support to the health and safety team, including but not limited to office works and document control. Can also write reports about the company's occupational Health and Safety to ensure seamless access across departments.
Check all the document on the occupational health and safety management system and advice their review to the responsible document holder.

The successful candidate will report to the **Safety Lead**
**Duty Station: Ngara**
**Roster: 6/3**
**Duties and Responsibilities**

- Ensure administration and management of the health & safety management system and attends general issues that are received, redirecting queries to members of the health and safety team as required.
- Follow up on Health & Safety training records, assist with course registration, issuing certificates as required.
- Process of accident / incident forms, PTO's, WPI, VFL and updating spreadsheets, follow up actions as required.
- Ensure a timely, accurate and efficient preparation and management of documents, control the numbering, sorting, filing and retrieval of both electronic and hard copy documents produced by the departments.
- Maintain quality assurance of all outgoing documentation, track, transmit and accurately file hard copy and electronic documents.
- Coordinate multi-office and work-sharing information in a timely manner.
- Develop and maintain a comprehensive filling system and computer database / system for all documents to be retained in the documentation in a control centre.
- Ensure that department documents are well managed, organizing an archiving system, retrieving documents upon request, and outlining a long-term storage strategy.
- Manage the operation of the document control centre to ensure that all users have the latest version of appropriate documentation in a timely manner.
- Organize and maintain a document control system, team meetings, solve safety issues, coordinate audits, and inspections, track corrective actions and incident data, review important safety documents and other duties that require a high degree of attention to detail.
- Assist in to make improvement and implement required changes relation to health and safety management system.
- Ensure compliance to applicable codes, legislation and procedures including health and safety.
- Interact and cooperate with all department members and ensuring support in filling and documenting work-related documents.
- Perform any other duties that may be required from time to time as directed by your supervisor / Manager.

**Qualifications**
- Certificate / Diploma in office administration.
- Relevant training certification to deliver role requirements.
- Three years administration, document control and office work experience.
- Any Health and Safety related qualifications.
- ISO Management system awareness training is an added advantage.

### COMMUNITY RELATIONS OFFICERS(RAP)-5

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit a Community Relations Officers - **RAP** to join the Tembo Nickel Project Team. **The CR Officers- RAP** will support the Community Relations and Social Performance Manager in implementing the Tembo Nickle RAP by promoting a clear understanding of the Tembo Nickel Resettlement implementation activities amongst the PAPs and local communities.

**This is a Fixed Term contract of 1 Year** and the successful candidate will report to the **CR RAP Lead**
**Duty Station: Tembo Nickel Project Site- Ngara**

**Duties and Responsibilities**
- Serve as liaison between TN and identified local stakeholders. Assist with key studies and research with a social aspect e.g., Environmental & Social Impact Assessment and Health Impact Assessment.
- Facilitate key Project work streams that have a community interface e.g., resettlement and exploration/surface drilling.
- Assist other Project departments (e.g., Security and Health, Safety & Environment) to identify and plan mitigation strategies for key social impacts.
- Write and submit all relevant reports (e.g., stakeholder engagement report, weekly report etc) to the Community Relations Lead for review and submission.
- Participate on development of department plans, monitoring, and evaluation of department activities.
- Jointly with Community Relations team, undertake monitoring, internal evaluation and documentation of all work done by CR Department.
- Undertake other duties as reasonably assigned by Community Relations Lead.
- In the absence of CRL the Senior Community Relations Officer will act as Community Relations Lead.

**Qualifications and Competencies**
- Advanced Degree in Social Sciences, Sociology, Social Anthropology, rural development, Environmental Sciences, or a related discipline, required.
- Minimum 5-7 years of professional experience working within rural communities in Tanzania required.
- Experience of investor financed Projects compliant with the International Performance Standards on land acquisition and livelihood restoration preferred.
- Minimum 5 years experience in, implementing and monitoring of Land Acquisition, Resettlement programs with specific experience on conducting land acquisition negotiations and agreements.
- Experience of overseeing execution of compensation payments and interfacing with banking institutions required.
- Excellent and proven data management skills and attention to detail required.
- Fluency in English and Swahili (written and spoken) essential.
- **Willingness to be based and work in an assigned Region is essential.**

**How to Apply**
Applicants are invited to send their resumes indicating the role tittle in the subject via email **jobs@tembonickel.com**

**Application closing date is 25th April,2023**
***Note:*** *We are committed to provide equal employment opportunities based on merit and we do not charge candidates any fees in the whole recruitment process.*

*Tembo Nickel offers a competitive remuneration package and ONLY shortlisted candidates will be contacted.*

***Women are strongly encouraged to apply.***

***For and on behalf of Tembo Nickel, Kabanga Nickel Project.***

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 'Dabi' Simba, Yanga imepita, akili zihamie robo fainali CAF

**HATIMAYE** mechi ya watani wa jadi 'Dabi' ya Kariakoo kwa timu kongwe zaidi nchini, Simba na Yanga, imepigwa jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa ni ya mzunguko wa pili baada ya ile ya raundi ya kwanza miamba hiyo kutoka sare ya bao 1-1 uwanjani hapo.

Miamba hiyo ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya soka la nchi hii, imetinga kwa pamoja robo fainali ya michuano ya kimataifa kwa msimu mmoja, ina kibarua kigumu kuelekea mechi zao zijazo kuweza kusaka tiketi ya kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba inayoiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa, itaikaribisha Wydad Casablanca ya Morocco katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa robo fainali utakaopigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Makapa.

Kwa upande wa Yanga yenye kibarua cha kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, itakuwa na shughuli pevu ugenini nchini Nigeria Jumapili wiki hii dhidi ya wenyeji wao, Rivers United katika mechi ya mkondo wa kwanza ya hatua ya robo fainali.

Ni mechi ambazo mashabiki wa soka wa timu hizo, lakini kwa kila Mtanzania mwenye mapenzi mema ya kuona mpira wa nchi hii ukipiga hatua, anataka kuona wawakilishi hao wa nchi kimataifa kwa ngazi ya klabu, wakipata matokeo mazuri na kusonga mbele zaidi.

Kwa mantiki hiyo, bila kujali matokeo ya mechi ya jana, ni wakati wa kila mmoja hususan wachezaji na mabenchi yao ya ufundi, kuyasahau na kuelekeza akili zao kwenye michuano hiyo ya kimataifa ambayo inaongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Kwa muda huu wa takriban siku tano zilizosalia kabla ya wawakilishi hao wa nchi kushuka dimbani, ni wakati wa mabenchi yao ya ufundi si tu kuwapa mbinu wachezaji na kufanyia kazi kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza kwenye mechi zilizopita, bali kuwajenga zaidi kisaikolojia ili kuweza kupata ushindi.


Ingawa wapo wanaoona kuna mlima mrefu kwa Simba kuweza kupenya kutokana na kupangiwa Bingwa Mtetezi wa michuano hiyo, Wydad Casablanca, lakini pia wakiamini Yanga ina nafasi kubwa ya kusonga mbele kutokana na ubora wa kikosi chao ukilinganisha na cha msimu uliopita ambacho kilitupwa nje na Rivers United kwenye Kombe la Shirikisho, lakini sisi hatuamini katika hilo kwani hatua kama hii timu zote ni bora.

Kadhalika, kwa Yanga kuamini tu wana kikosi bora pasipo kujipanga vizuri na kuwaheshimu Rivers United wakiwa kwao, wanaweza kujikuta wakibebeshwa mzigo mkubwa na mechi ya marudiano kuwawia vigumu 'kupindua meza'.

Aidha, ikumbukwe Rivers United hiyo, nayo ilianzia Ligi ya Mabingwa kabla ya kutolewa na Wydad Casablaca kwenye raundi ya kwanza, hivyo kuangukia Kombe la Shirikisho kama ilivyo Yanga ambayo iliondoshwa na Al Hilal ya Sudan, hivyo si timu ya kuibeza hata kidogo.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba ikiwa nyumbani katika mechi ya mkondo wa kwanza dhidi ya Wydad iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 kabla ya kwenda kuangukia pua ugenini kwa kipigo cha mabao 6-0 nchini Morocco, hivyo Yanga inapaswa kujipanga vilivyo na si kuibeza.

Sisi tunaamini wawakilishi wetu hao, Simba na Yanga, wakijipanga vizuri na kucheza kwa kujiamini huku wakiwaheshimu wapinzani wao, wanaweza kabisa kupata matokeo mazuri na kusonga mbele nusu fainali na hata fainali, hivyo kwa siku hizi chache ni wakati wakusahau matokeo ya mechi ya jana na zilizopita na kisha kujipanga vema kwa mechi hizo za kimataifa.






## Muungwana Lazima Nilonge

# Usajili bora michuano CAF unatakiwa ufanyike sasa

Na Adam Fungamwango

**KUMEKUWA** na taarifa ambazo hazijathibitishwa kwa pande zote kuwa kipa namba mbili wa Klabu ya Simba, Beno Kakolanya amefikia makubaliano na Singida Big Stars kwa ajili ya kuichezea timu hiyo msimu ujao.

Mpaka sasa hakuna klabu kati ya hizo mbili iliyokubali au kukanusha, lakini vyanzo kutoka ndani ya Simba pamoja na dalili zinaonesha kuwa kipa huyo huu ni msimu wake wa mwisho kukipiga Msimbazi.

Kama ni kweli kwamba tayari Singida Big Stars wameipata saini ya kipa huyo, watakuwa wamelamba dume na nawapa kongole kwa kuamua kuanza kufanya usajili wa haraka sana.

Kwa asilimia kubwa ni kwamba Singida Big Stars msimu ujao ni moja kati ya timu itakayoiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, hivyo wameanza kusaka wachezaji wenye viwango vya kucheza mechi za kimataifa pia wakianza na langoni.

Vyovyote itakavyokuwa, lakini hii ni kengele kwa klabu zingine ambazo zina nafasi kwa msimu ujao kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kuanza kufanya usajili mapema kwa ajili ya kutengeneza vikosi vyao.

Singida Big Stars ambayo ilipanda daraja msimu huu ni klabu inayoshangaza kidogo, kwani pamoja na uchanga wake, lakini imeonyesha iko vizuri kwenye masuala ya utawala, hasa katika kusaka wachezaji bora na wenye vipaji, na sasa wameanza kujitofautisha tena kwa kuanza kujiandaa mapema na usajili.

Ni moja kati ya klabu zilizofanya usajili bora zaidi msimu huu hapa nchini, ikiwa na wachezaji ambao hata klabu kubwa kama Simba, Yanga na Azam zinawamezea mate. Cha ajabu ni kwamba wengi hawakuwa wanajulikana kabla, na wala hawajachafua kurasa za magazeti na mitandao, badala yake kazi zao zinaonekana uwanjani zaidi kuliko kwenye midomo ya watu. Wanaonekana kuwa wana maskauti wazuri zaidi.

Sipati picha sasa kwenye usajili wa wachezaji ambao watakwenda kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Hili ni somo kwa Klabu za Simba, Yanga na Azam nazo kuanza kusajili wachezaji kwa msimu ujao, badala ya kusubiri ligi zote zimeisha, halafu ndiyo zinaanza kutafuta wachezaji ambao wamepandishwa gharama na mawakala, baada ya kuanza kutaka kunyang'anyana.

Afrika hii ina wachezaji wengi mno wenye vipaji, lakini klabu zetu zimeshindwa kabisa kuwa na maskauti wazuri, badala yake wamekuwa na kundi la wachezaji wachache tu walioonekana wakicheza dhidi yao na kuanza kugombania, tena kila msimu utasikia majina ya watu hao hao tu.

Hata Bara la Amerika Kusini kama Brazil, Peru, za zingine kuna wachezaji wenye vipaji kwa gharama za kawaida tu, shida ni wigo wa mawakala wao. Kina Bruno Gomes wapo wengi sana, lakini wanahitajika watu kama viongozi wa Singida Big Stars kuwapata.

Kwa klabu kama Simba, Yanga na Azam kwa muda huu zilitakiwa tayari zimeshajua mwakani zinamsajili nani kuongeza nguvu kwenye kikosi chao kwa kuwapa mikataba ya awali, na ligi zinapomalizika, basi nao wanamaliza shughuli kwa kuwasainisha mikataba halisi.

Hii inasaidia sana pale msimu wa kujiandaa na mashindano 'pre-season' inapoanza, kuwa na wachezaji wote wanaohitajika, badala ya kukaa kambini na wachezaji wanaokuja kuachwa baadaye, wanasajiliwa wengine ambao hawana utimamu wa mwili kwa wakati huo. Hili limeathiri sana Simba kwa misimu miwili sasa, kwani inachelewa sana kusajili, badala yake inaingia kambini kujiandaa na msimu na wachezaji wengine ambao baadaye wanakuja kuachwa au kutolewa kwa mkopo, lakini wale waliotakiwa kukaa na kocha akiwapa ufiti na mbinu, wanasajiliwa baadaye kabisa siku zimeisha kiasi cha wachezaji wao kutokuwa na utimamu, wakihitaji muda mrefu mno ili kuwa kwenye viwango vyao na wakati huo michuano inakuwa imeshaanza.

Tena kwa safari hii wanacheza Super Cup itakayoanza Agosti, hivyo wanatakiwa wabadilike sana. Msimu ujao timu nne zinazoiwakilisha nchi zijaribu kubadilika, zisajili mapema ili wakati wanakwenda 'pre-season' wawe tayari na wachezaji wote wa msimu husika, badala ya kusajiliwa wakati kipindi hicho kimemalizika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## HABARI KITAIFA

# TANROADS kutekeleza miradi mitano barabara Morogoro

**Na Mary Geofrey**

WAKALA wa Barabara nchini (TANROADS), unatarajia kutekeleza miradi mitano ya ujenzi wa barabara mkoani Morogoro.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Morogoro, Alinanuswe Kyamba, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema wanatarajia kutekeleza miradi hiyo ambayo itawezesha kuunganisha wilaya zote za mkoa huo kwa kiwango cha lami na kuinua uchumi wa wananchi wa maeneo hayo.

Alisema miradi yote zabuni zake zimeshatangazwa na iko katika hatua za mwisho ili kusaini mikataba.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni wa Barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere yenye urefu wa kilomita 11.6, Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Taweta - Madeke, sehemu ya Ifakara - Mbingu, Kilomita 62.5.

"Pia kuna mradi wa ujenzi wa Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Taweta - Madeke, sehemu ya Mbingu - Chita JKT, yenye urefu wa Kilomita 37.5," alisema.

Aliutaja mradi mwingine ni wa Barabara ya Bigwa - Kisaki (sehemu ya Bigwa -Mvuha, kilomita 78, pamoja na madaraja ya Ruvu na Mvuha.

Mradi mwingine ni wa Barabara ya Ifakara - Lupiro - Mahenge / Lupiro - Malinyi - Kilosa kwa Mpepo - Londo - Lumecha na Malinyi JCT - Malinyi, kilomita 422.54.

Aidha, alisema ujenzi wa Barabara ya Mikumi- Ifakara kwa kiwango cha lami hadi sasa umefikia asilimia 78.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo unaohusisha pia ujenzi Daraja la Ruaha Mkuu unatarajiwa kukamilika Oktoba, mwaka huu.

"Hadi kufikia Aprili 2023, utekelezaji wa mradi kwa ujumla ulikuwa umefikia asilimia 78, kwa sasa mkandarasi amekamilisha kilomita 43 za lami na kazi zingine zinaendelea kwa hatua nzuri."

Alisema madaraja yote yameshakamilika kwa asilimia 83 na Daraja la Ruaha Mkuu kilichoalia ni kukamilisha kitako cha juu.

Alisema kukamilika kwa Daraja la Ruaha Mkuu kutafanya magari mawili kupita kwa wakati mmoja tofauti zamani.

Kyamba alisema mradi huo ulianza mwaka 2018, lakini matatizo mbalimbali ikiwamo mvua imekuwa sababu ya kuchelewa kukamilika kwa wakati.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika Tanzania, Adam Mihayo (kulia), akiwaongoza wateja kupata futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake wa Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba mbaroni tuhuma kumnajisi mtoto wa kambo, akiri vilevi vinamsababishia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MSEVENI Mchele (40) mkazi wa Mtaa wa Nyasubi, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wake wa kufikia mwenye umri wa miaka 12, mwanafunzi wa darasa la saba.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa halmashauri hiyo, Abrahaman Nuru, aliwaambia waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 13, mwaka huu, nyumbani kwa mtuhumiwa baada ya mke wake kusafiri kwenda mkoani Morogoro kwenye matibabu ya afya yake.

Alisema mtuhumiwa alitumia nafasi hiyo na kumlaghai mtoto huyo kwa kumnunulia chipsi na kumlewesha pombe na kisha kumnajisi.

Nuru alisema, kwa kushirikiana na jeshi la polisi walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo baada ya majirani zake kusikia kila siku kelele za mtoto akilia ndani kwa maumivu ya kufanyiwa kitendo hicho na kutoa taarifa kwa mama yake mdogo na kuamua kuweka mtego ambao ulimnasa na kumkamata mtuhumiwa. Alisema, baada ya tukio hilo walimpeleka mtoto hospitali kumpima afya yake na daktari alithibitisha kuingiliwa zaidi ya mara moja, hata hivyo hakuwa na maambukizi wala mimba.

Ofisa huyo alisema mtoto alipohojiwa alikiri kufanyiwa ukatili na baba yake na kupata maumivu makali.

"Kwa sasa binti huyo amechukuliwa na mama yake mkubwa anayeishi mkoani Shinyanga na tunafanya taratibu za kumhamisha shule ili akaendelee na masomo yake, hapa hawezi baada ya kuathirika kisaikolojia," alisema.

Katika mahojiano mtuhumiwa alikiri kutenda kosa hilo kwa madai kuwa anatumia vilevi ambavyo vinamsabishia kufanya matukio ambayo hakuyatarajia na kuomba kusaidiwa ili suala hilo liweze kumalizika.

Shekhe wa Wilaya ya Kahama, Alhaj Omary Damka, akiwa anazungumza na wanawake wa dini ya Kiislamu aliwataka kutowaamini waume zao kwa kuwaacha na watoto wa kike wenye umri mkubwa kwa kuwalea kwa kuwa wanaweza kukumbana na matukio ya ukatili ikiwamo kubakwa au kulawitiwa.

Pia, aliwataka kutowachanganya wageni wa kiume au wakike na watoto wao wanapowatembelea katika familia zao ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili wa kijinsia na kujenga tabia ya kukaa pamoja na watoto na kuwasikiliza matatizo yao na kuyatatua kwa wakati hususani watoto wa kike.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alisema, vitendo hivyo havitavumilika na pale wahusika wanaobainika kutendo vitendo hivyo atahaklikisha wanawajibishwa kisheria ili iwe fundisho kwa wengine na kuwataka viongozi wa dini kukemea hayo kila siku za ibada.


## KUPOTEA KWA CHETI



**LILIAN CHARLES MWAKISYALA** Anatangaza kupotea kwa cheti cha ngazi ya **DIPLOMA IN THEOLOGY** chenye Index namba **TU/IUCO/038448** kilichotolewa chuo kikuu kishiriki IRINGA mwaka 2011 kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi POLISI TAARIFA. **IRI/IRI/163954/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA BUKOBA**
**KITUO CHA BUKOBA MJINI MKOA WA KAGERA**
**Shauri la Madai /Ndoa Na. 2023**
**Jina la Mdai ........................JULIUS M. KASHUBAO**
**Jina la Mdaiwa ..................ADRIANA N. SOSTHENES**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa ADRIANA N. SOSTHENES**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao ya talaka, Unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 24 Mwezi 04 Mwaka 2023 saa 8:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 05 Mwezi 04 Mwaka 2023.

HAKIMU

38

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Wilaya ya Bukoba**
**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera**
**Shauri la Madai/ Ndoa Na. 14/2023**
**Jina la Mdai .................Bonephace Oigen Ngonyani**
**Jina la Mdaiwa ................Stahimili Charles Nyigu**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Kwa **STAHIMILI CHARLES NYIGU**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/ Wameleta madai yake/ yao ya Talaka. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 21 Mwezi 04 Mwaka 2023 saa 8:00 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 14 Mwezi 04 Mwaka 2023.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELISHA AMELYE CHENGULA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA DYNA** yenye usajili namba **T162 AMQ ,** CHASSIS NAMBA: **BU888009975** na ENGINE NAMBA: **14B12400998.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MKB/RB/50/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA.**
**KITUO CHA KARABAGAINE**
**MADAI YA TALAKA NO. 03/2023**
**JASILATH YASSIN ............................MDAI**
**DHIDI YA**
**KELVIN BENARD ....................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

Kelvin Benard unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii tarehe 27/04/2023 saa 2:30 Asubuhi kuja kujibu madai haya ukiwa na shahidi wako.

Kwa kuwa ni siku ya kukata shauri fika na hati zote zinazohusiana na shauri hili na kama hautahudhuria shauri hili litaendelea kusikilizwa upande mmoja.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Mhuri wa mahakama hii.

**C. R. RICHARD**
**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

LEONARD GEORGE NYENSHILE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA SUZUKI ESCUDO YENYE NAMBA ZA USAJILI T 209 AHT YENYE CHASSIS No. TDOIW280585 NA ENGINE No. G16A431702 KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI: TAARIFA YA POLISI KAH/TR /RB/235/2023.

# Shirika lashauri uharaka mabadiliko Sheria ya Ndoa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imeshauriwa kuharakisha kufanyika kwa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa 1971 katika Bunge la Bajeti linaloendelea ili kuweka umri wa miaka 18 kama umri wa chini wa kuolewa na kuoa na kuongeza kipengele cha kumaliza elimu ya msingi na sekondari.

Ushauri huo umetolewa na Mkurugenzi wa Shirika la Padeko, Wilbard Mwinuka, wakati akizungumza na Nipashe, alisema kuwa kwa mujibu wa sheria mtu mzima ni kuanzia miaka 18.

"Sisi kama shirika tunatambua kwamba mtu mzima ni yule ambaye amemaliza elimu ya msingi na sekondari, lakini yule mwenye miaka 18 na kuendelea, kwa hiyo sisi tunapenda kupendekeza na tunaiomba serikali ipitishe kwamba mtu wa umri kuanzia miaka 18 na kuendelea ambaye amekwisha kumaliza elimu ya msingi na sekondari ndio aruhusiwe kuolewa na sio chini ya miaka 18," alisema Mwinuka.

Aidha, alisema kuwa imezoeleka msichana akimaliza darasa la saba na asipofaulu kwenda sekondari basi anaishia kuolewa.

"Maeneo ya kijijini asipofaulu kwenda sekondari ni kama mtu mzima anaweza akawa na miaka 15, lakini kiuhalisia kwa sababu ya kiumri nafikiri sheria isiweze kuruhusu,huyu anauhitaji bado kujifunza hata kama nje ya mfumo wa sekondari,anahitaji kujifunza pia maisha bado ajakuwa ni mtoto anaakili za kitoto nafikiri ni muhimu sana akafikisha miaka 18 na kuendelea," alisema Mwinuka.

"Hata kibaiolojia, afya inashauriwa mtu kuanzia 18 na kuendelea anakuwa mwili wake umekaa vizuri anaweza akapokea ujauzito na anazaa katika usalama mzuri kuliko yule ambaye atazaa kwenye miaka pungufu ya hiyo," alisema.

Alisema mila na desturi pia zinachangia ndoa za utotoni na kwamba hazitakiwi kufumbiwa macho wala kuungwa mkono.

"Mi nafikiri serikali ione haja na umuhimu wa kutambua miaka 18 na kuendelea ndiyo umri wa mtu mzima na hivyo ndiye aweze kuwa anaruhusiwa kuolewa na mtu aruhusiwe kuoa mtu wa namna hiyo akiwa pia amemaliza elimu yake ya msingi na sekondari kwa sababu tusipotaja pia kumaliza elimu mtu ataona kwamba yule si ameshamaliza tayari kwa ajili ya kuolewa, lakini yupo ambaye yupo form five anaumri wa miaka 19 huyu ni mwanafunzi hivyo kipengere cha elimu kiwe cha muhimu," alisema Mwinuka.



Ofisa Raslimaliwatu wa Barrick Bulyanhulu, Alpha Gonzi, akizungumza na wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo lililoandaliwa na taasisi ya kuchipua na kuendeleza vipaji vya uongozi kwa vijana AIESEC kwa udhamini wa kampuni ya Barrick katika ukumbi wa Nkurumah wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MNH yazindua maabara kupima magonjwa ya damu

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imezindua maabara ya kisasa yanye mashine itakayokuwa na uwezo wa kufanya vipimo vya magonjwa ya damu, uwezo wa kupima sampuli 180 kwa saa.

Akizungumza jana baada ya kutembelea maabara hiyo, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu alisema magonjwa ya damu awali yalikuwa hayagunduliki mapema kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo uchache wa vifaa.

Alisema uwapo wa maabara hiyo utaongeza uwezo wa upatikanaji huduma za magonjwa ya damu, ikiwamo himofilia, selimundu, kwa kuwa utambuzi wa mapema kwa wanaougua ndivyo urahisi wa matibabu unavyowezekana.

"Wagonjwa wa himofilia wao shida kubwa ni kuvuja damu, na ilikuwa huwezi kuwafanyia upasuaji na kumudu uvujaji damu. Lakini sasa wataalamu wamepewa mafunzo pamoja na madaktari, wauguzi, ili kutoa huduma sahihi kwa wagonjwa hawa," alisema Prof. Nagu.

Kadhalika aliitaka MNH, kuendelea kuzijengea uwezo hospitali za kanda, rufani na mikoa, ili huduma kama hizo zitolewe pale wagonjwa walipo, badala ya kuzifuata MNH.

Prof. Nagu alisema kwa sasa unaandaliwa mwongozo na utakamilika hivi karibuni ambao utabainisha hatua za matibabu za magonjwa ya damu pamoja na kuwaongoza watoa huduma na uhakika wa usalama.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu kutoka MNH, Dk. Stella Rwezaura, alisema Siku ya Himofilia Duniani, iliyoadhimishwa jana inakumbusha umuhimu wa kubaini wagonjwa hao. "Ugonjwa huu (himofilia) wa kuvuja damu ni ugonjwa kama magonjwa mengine na mtu anazaliwa nao. Ila watu walio wengi wanaamini mtu karogwa na wanaishia kwa waganga wa kienyeji. Hadi sasa kati ya watu 6,300 wanaougua nchini ni 200 wamefikiwa," alisema.

Dk. Rwezaura ambaye pia ni Mratibu wa mradi wa kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma za magonjwa ya damu, alisema ipo kazi kubwa ya kuongeza uelewa na kliniki za upimaji magonjwa hayo, kwa siku MNH hupima kati ya 10 hadi 20.

"Kliniki yetu MNH haina mapumziko kwa sababu mtu anakuja tayari anavuja damu, hatuna kliniki ya njoo kesho au baada ya wiki, utakuta ameamka leo anavuja damu, anahitaji huduma. Tumetoa mafunzo kwa wataalamu, wagonjwa na wazazi," alisema Dk. Rwezaura.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, MNH, Dk. Jessie Mbwambo, alisema ujumbe wa mwaka huu kwenye maadhimisho hayo ni; 'Zuia kumwaga damu, zuia athari zitokanazo na magonjwa ya damu, ikiwamo ulemavu na vifo'.

# Mradi kumaliza tatizo ukosefu maji Boko Mnemela

**Na Joseph Mwendapole**

WAKAZI 1,600 wa Boko Mnemela, Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani, wanatarajia kunufaika na majisafi na salama unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ambao uko mbioni kukamilika.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Charles Stephen, kupitia mkoa wa kihuduma DAWASA Kibaha.

Alisema utekelezaji wa mradi unaendelea kwa kasi, umehusisha ulazaji wa bomba za inchi 6,8 na 12 kwa umbali wa kilomita tatu kwa gharama ya Shilingi milioni 156.

Alisema kazi hiyo iliyoanza kutekelezwa Septemba mwaka jana, inatarajiwa kumalizika mwishoni wa mwezi huu, na utawanufaisha wakazi zaidi ya 1,600 wa Boko Mnemelea, Boko Temboni, Mwanalugali na Boko Timiza.

"Tuko kwenye hatua nzuri mpaka sasa, ulazaji wa mabomba unaendelea tunaimani mradi huu unaenda kuwa mwarobaini wa tatizo la upatikanaji wa maji iliyopo kwa mda mrefu," alisema.

Alisema mradi huo umetokana na tatizo la ongezeko la wakazi na mahitaji kuzidi uwezo na uchakavu wa miundombinu iliyoshindwa kupeleka maji kwenye Kata ya Boko Mnemela na viunga vyake.

Mwenyekiti wa Kata ya Boko Mnemela, Jumanne Msusa, aliiomba DAWASA kusimamia kikamilifu kuhakikisha huduma inapatikana kwa wakati ili wananchi waanze kufaidika na huduma ya majisafi.

"Kwa kweli tunaona jitihada na tunapongeza sana, kilio chetu sisi ni maji tutafurahi zaidi tukiona wananchi wanaanza kupata huduma, hivyo niwaombe DAWASA msituangushe hakikisheni mradi unakamilika kwa wakati," alisema Msusa.

Fransisca Kajembe, alisema anamatumaini makubwa kilio chao kinaenda kwisha kwani wameteseka kwa mda mrefu bila mafanikio, kuanzia kutafuta maji mbali na makazi yao na kwa gharama kubwa.

"Tumeteseka sana kupata huduma kwenye eneo hili, DAWASA tunashukuru kwa jitihada hizi zinazoendelea tunataka tuondokane na adha hii" alisema Kajembe.

Mradi wa maji Boko Mnemela ni mojawapo wa miradi ambayo DAWASA imekabidhiwa kutoka kwa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa lengo la kuuboresha ili huduma ipatikane kikamilifu.



# MAIPAC lagawa vitabu kwa wakurugenzi wa mashtaka

**Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Wanahabari la Kusaidia Jamii za Pembezoni (MAIPAC), limegawa vitabu vya maarifa ya asili katika utunzaji wa mazingira, vyanzo vya maji na misitu kwa wakurugenzi wa mashitaka wasio wa serikali.

Wakurugenzi wa mashirika hayo ambayo ni wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binaadamu (THRDC) walitembelea MAIPAC kujifunza utendaji kazi wake.

Wakurugenzi na wawakilishi wa mashirika hayo waliongozwa na Mkuu wa Dawati la Wanachama la THRDC, Lisa Kagaruki.

Wawakilishi wa mashirika hayo licha ya kutembelea MAIPAC, pia walipatiwa vitabu vya maarifa ya asili katika utunzaji wa mazingira, vyanzo vya maji na misitu ambavyo vimeandaliwa na shirika hilo kwa kushirikiana na Shirika la Elimu ya Urai na Msaada wa Kisheria (CILAO), kwa udhamini wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), kupitia programu ya miradi midogo na mfuko wa mazingira duniani (GEF).

Vitabu hivyo vilizinduliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Muungano, Dk.Selemani Jafo, vimekuwa vikiombwa na wadau mbalimbali wa mazingira na tayari vimesambazwa katika maeneo kadhaa nchini ikiwepo shuleni.

Vitabu hivyo ni sehemu ya mradi wa uhifadhi wa mazingira, vyanzo vya maji na misitu kwa maarifa ya asili ambao umetekelezwa katika Wilaya ya Monduli, Longido na Ngorongoro.

Mkurugenzi wa MAIPAC, Mussa Juma alisema MAIPAC ni taasisi ya wanahabari ambao wamekuwa wakiandika habari juu ya jamii za pembezoni.

Alisema hadi sasa kuna wanahabari 86 ambao ni wanachama ambao wako katika mikoa ya Manyara,Mara, Dodoma, Dar es salaam, Pwani, Kilimanjaro, Singida, Mwanza, Shinyanga, Morogoro na Arusha

Vilevile alisema pia kuna wanachama ambao siyo wanahabari lakini ni wadau wa masuala ya haki ardhi, mazingira na usaidizi wa jamii za pembezoni.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa vitabu hivyo, Mratibu Dawati la Wanachama wa THRDC, Lisa Kagaruki, alipongeza shirika hilo kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Alisema shirika hilo ni mwanachama wa muda mrefu wa THRDC na limekuwa likifanya vizuri katika utekelezaji wa miradi yake kwa kutumia vyombo vya habari.

Aidha, alisema licha ya kutoa kitabu hicho pia wamekuwa wakifanya kazi nzuri katika kufuatilia haki za binaadamu nchini hasa katika makundi ya jamii za pembezoni na katika vyombo vya habari.

Mkurugenzi wa Shirika la PWY kutoka mkoani Mtwara, Alfred Muttakakwa, alilipongeza shirika hilo kwa kazi nzuri ikiwamo kuchapisha kitabu cha maarifa ya asili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Community Hands Foundation (CHF) ya jijini Dar es Salaam, Paul Makoe, alipongeza kazi nzuri kazi zinazofanywa na shirika hilo.

Makoe alisema CHF na MAIPAC wana uhusiani mkubwa ikiwemo kushirikiana katika masuala kadhaa ya utendaji na kupata wahisani.

# Jela maisha kwa kumbaka mtoto wa miaka 15 Babati

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imemhukumu kifungo cha maisha jela mkazi wa Kijiji cha Ngolay, Peter Roberth (20) kwa kosa la kubaka na kumnajisi mtoto wa miaka 15 (jina limehifadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Jumaa Mwambago.

Akisoma hukumu hiyo hakimu Mwambogo alisema mshtakiwa ametiwa hatiani baada ya kukutwa na makosa mawili ya kubaka na kunajisi mtoto wa miaka 15.

Hata hivyo hakimuMwambogo alisema mshtakiwa alitenda makosa hayo Agosti 15 mwaka jana katika Kijiji cha Ngolay, katika Kata ya Mwada wilayani Babati mkoani humo.

Aidha, alisema mshtakiwa alikiuka kifungu cha 130(1)(2)(c) kwa kosa la ubakaji na kifungu cha 131(1) vya kanuni ya adhabu sura ya 20 kama vilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Hakimu Mwambago alisema amemtia hatiani mshtakiwa huyo baada ya kusikiliza ushahidi uliotolewa mahakamani kwa pande zote mbili na mashtaka yalithibitishwa pasipo kuacha shaka.

Vilevile alisema mahakamani hapo kuwa upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi watano na vielelezo viwili ambavyo vimeisaidia Mahakama kumtia hatiani na kutenda haki.

Kadhalika alisema ushahidi uliotolewa mahakamani umeonyesha kuwa mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi wadarasa la saba alifanyiwa unyama huo na baba yake mdogo.

Naye Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Emmanuel Jumbe, kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwa watu wanaofanya ukatili wa aina hiyo



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, akipanda mti kwenye kata ya Naisinyai jana, kupitia mradi wa kusaidia kaya masikini (TASAF) wa kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tanzania ya kwanza duniani kuwa na simba wengi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa amesema Tanzania inashika nafasi ya kwanza duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya simba.

Aliyasema hayo juzi jijini Arusha wakati akizindua Chama cha Wakala wa Usafirishaji Watalii Wanawake Tanzania (TAWTO).

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), zinaonyesha kuwa idadi ya wanyamapori hapa nchini inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

“Sisi serikali kwa takwimu za wanyamapori tulizonazo za hivi karibuni zinaonyesha idadi ya simba tulionao ni zaidi ya 17,000, hivyo kwa idadi hii inafanya nchi yetu kuwa ya kwanza duniani kuwa na wanyama aina ya simba kuliko taifa lolote,”alisema.

Kadhalika alisema wizara hiyo imejipanga kufanya mapitio ya sera na sheria ili watu wanofanya shughuli za utalii waweze kuutangaza utalii kwa njia tofauti pamoja na wafanye kazi katika mazingira mazuri na wezeshi.

Alisema kupitia Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999 imetilia mkazo suala la utalii endelevu kwa kutambua mchango wa wadau mbalimbali zikiwamo sekta binafsi na wanawake.

Hata hivyo alisema hivi karibuni kumekuwapo na ongezeko kubwa la wanawake wanaojishughulisha na shughuli za utalii wakiwamo waongoza utalii, wakala wa usafirishaji wa utalii, waendesha utalii, askari wa uhifadhi na wahudumu wa malazi katika hoteli za kitalii.

Aidha, aliwataka kuzingatia Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008, kanuni na utaratibu za kuendesha shughuli za utalii nchini ikiwamo kulipa kodi ya serikali wakati wakitekeleza majukumu yao ya kikazi.


Pia alisema kuwa wizara hiyo kwa kushirikina na wataalamu wake wamefungua milango ya kusikiliza kero zinazowakabili wadau na vyama vyote vya utalii.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk.Hassan Abbas, alisema kupitia Filamu ya The Royal Tour Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa ya kutangaza utalii na vivutio vilivyoko nchini.

Alisema pia kuanzishwa kwa TAWTO ni matokeo ya filamu hiyo kwa kuwa ilitoa fursa kwa watu mbalimbali duniani kuifahamu nchi.

Mwenyekiti wa TAWTO, Elizabethi Mwakajila, alisema lengo la kuanzishwa kwa chama hicho ni kuhamasisha wanawake kushiriki katika uendelezaji wa sekta ya utalii na kuitangaza.

Alitumia fursa hiyo kuiomba Wizara ya Maliasili na Utalii, kuwapata ushirikiano wakati wa utekelezaji wa kazi zao.





# Vikundi 82 vilivyoshindwa kufanya marejesho vyafikishwa mahakamani

**Na Alex Sayi,** MASWA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Maswa imevifikisha mahakamani vikundi 82 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutokana na kushindwa kurejesha mikopo ya asilimia 10 ya Sh. milioni 129.9 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani wilayani Maswa ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Shanwa, Poul Maige, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu. Maige alisema kuwa baraza hilo tayari lilishaelekeza kufikishwa mahakamani vikundi vyote vilivyoshindwa kurejesha mikopo hiyo ambayo ilikopwa na kushindwa kuirejesha hali inayowakosesha waombaji wengine wenye uhitaji wa mikopo katika halmashauri.

Alisema baada ya baraza kutoa uamuzi huo, ofisi ya ofisa maendeleo pamoja na ofisa mikopo wanashughulikia suala hilo kwa kuwa bajeti ya 10% inayotengwa na halmashauri kila mwaka haitoshelezi kuvikopesha vikundi vyote.

Kuhusu ukusanyaji mapato, alisema wanatarajia kukusanya zaidi ya Sh.bilioni nne kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na makadirio ya bajeti ya Sh.bilioni 2.2 kwa mwaka wa fedha uliopita 2021/2022. Mgurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Saimon Berege alisema kuwa mashauri ya vikundi 50 yalifikishwa mahakamani kati ya vikundi 82 na tayari zaidi ya Sh.mil 98.4 zimeshalipwa.

"Pamoja na fedha hizi kurejeshwa bado tuna uhaba wa bajeti hata hivyo bado tunaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 tumetenga zaidi ya Sh.mil 300 kwa ajili ya makundi ya wanawake, vijana na walemavu,"alisema.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii wilayani humo, Rodger Limo alisema kwa mwaka wa fedha 2021/2022 zaidi ya Sh.milioni 200 zilikopeshwa kwa vikundi 25 kati ya vikundi 80 vilivyoomba mkopo.



Ofisa Mpima Ardhi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, John Solo (kulia), akishirikiana na wananchi wa kijiji cha Nyabilongo, kata ya Kwehancha, kuweka alama namba 248 ambayo ndio kubwa kwa ajili ya kutambua mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENEPA) kwa upande wa Wilaya ya Tarime, mkoani Mara mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Prof. Mahalu: Somo la haki za binadamu lifundishwe kuanzia awali

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAKAMU wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT), Balozi Costa Mahalu ameishauri serikali kuongeza somo la haki za binadamu katika mtaala wa elimu kuanzia awali mpaka vyuo vikuu, lengo ni kuongeza wigo wa uelewa wa haki hizo katika jamii.

Alitoa ushauri huo juzi wakati akishiriki utiaji saini wa mkataba wa ushirikiano wa utoaji elimu na utekelezaji wa haki za binadamu baina ya SAUT na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) uliofanyika chuoni hapo.

Alisema kwa sasa ni vyema serikali ione umuhimu wa kulitazama suala hilo kwa kueneza elimu hiyo kuanzia awali kwa lengo la kuhakikisha watoto wanaanza kuelewa haki zao wenyewe.

"Elimu kama hii isitolewe vyuo vikuu pekee bali hata huku chini wazitambue haki zao pamoja na wenzao waelewe uhusiano wao pamoja na wenzao , heshima yao pamoja na ulazima wa kuheshimiana wao kwa wao na kuelewa kuwa usipo mheshimu mwenzako tayari umemvunjia heshima," alisema Prof.Mahalu

Mkurugenzi wa THRDC, Onesmo Ole Ngurumwa alisema wanafunzi wanatakiwa kuandaliwa mapema kuzijua haki za binadamu ili ziwasaidie hata wakiwa maeneo ya kazi.

Alisema hali ya kushindwa kutambua haki za binadamu kwa vijana mara kadhaa imekuwa ikisababisha kutokea kwa matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuporomoka kwa maadili ya Watanzania.

"Wanafunzi wengi wamekuwa wakihitimu mpaka ngazi ya vyuo vikuu bila kuwahi kukutana na suala lolote linaloitwa haki za binadamu na hao hao ndiyo tunaowakuta katika sehemu mbalimbali za utoaji haki hizo hali inayosababisha watu hao kuzivunja bila ya kuelewa," alieleza Ngurumwa

Elizabeth Hosea ni mwanafunzi katika chuo hicho alisema hatua ya chuo hicho kuingia mkataba wa ufundishaji na utoaji wa elimu ya haki za binadamu utawasaidia katika kuhakikisha wanakuwa na weledi katika utendaji kazi wao wakati wote wawapo shuleni pamoja kazini.

# Mawakala wa usajili bidhaa kupewa tuzo

**Na Ibrahimu Mmamba,** SAUT

KAMPUNI ya Vodacom Tanzania imezindua programu maalumu ya kutoa tuzo na zawadi kwa mawakala wa usajili wa bidhaa zao ikiwamo kwenda Afrika Kusini mwisho wa mwaka huu, kama sehemu ya motisha ili kuendelea kufanya kazi kwa weledi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa programu hiyo juzi Jijini Mwanza, Mkurugenzi wa Biashara na Masoko wa Vodacom Tanzania, Linda Riwa alisema hatua hiyo ni sehemu ya kutambua mchango wao katika kuhudumia jamii.

"Tunajivunia kuendelea kuwa kampuni bora ya teknolojia na mawasiliano kupitia ubunifu wa kidijitali unaonufaisha jamii ya Watanzania nchini kote. Leo tunapenda kutambulisha programu yetu mpya ijulikanayo kama "Vodacom Stars' inayolenga kuwanufaisha mawakala wetu wa usajili, ikiwa ni sehemu ya kuwashukuru kwa kuwa wanafamilia wa Vodacom na vile vile kuwawezesha kiuchumi kwani Vodacom ni zaidi ya mtandao," alisema Riwa.

Riwa alisema kupitia programu hiyo mawakala watajipatia fursa ya kujishindia zawadi mbalimbali ikiwemo safari ya kwenda Afrika ya Kusini itakayogharamiwa kila kitu na Vodacom Tanzania.

Alitaja zawadi nyingine ni pikipiki, baiskeli, spika za muziki, bima ya afya, majiko ya gesi ya kupikia, luninga, simu za mkononi na magodoro.

Mkuu wa Kanda ya Ziwa wa Kampuni hiyo, Ezekiel Nungwi, alisema kuwa ili kuhakikisha mawakala wa usajili wanawafikia wateja na kuwafikishia huduma za kimtandao watakuwa na shughuli mbalimbali katika viunga tofauti vya mikoa mbalimbali nchini.

Alieleza shughuli hizo kuwa ni pamoja na uhamasishaji kupitia magari yenye vipaza sauti, kuwatembelea mawakala na wafanyabiashara, pamoja na kuzungumza na wateja mitaani ili kuwaelimisha kuhusu huduma na bidhaa zetu na kuwaunganisha ili waweze kunufaika nazo.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 5 WANAOFANANA KUCHEZA NA LIONEL MESSI UK. 12-13



"Nilifika kwa basi nikaondoka na Bugatti" amefichua Georgina Rodriguez jinsi maisha yake yalivyobadilika baada ya kukutana kwa mara ya kwanza na Cristiano Ronaldo.

# GEORGINA NA SIMULIZI MAISHA NA RONALDO



**MADRID,** Hispania

"NILIFIKA kwa basi nikaondoka na Bugatti" amefichua Georgina Rodriguez jinsi maisha yake yalivyobadilika baada ya kukutana kwa mara ya kwanza na Cristiano Ronaldo.

Mwanamitindo huyo wa Hispania, Georgina, alifunguka kuhusu tarehe yake ya kwanza ya kukutana na Ronaldo na mabadiliko yaliyofuata katika maisha yake.

Mhispania huyo alikuwa akifanya kazi katika duka la nguo la Gucci mjini Madrid, ambapo ndipo alipokutana na Ronaldo kwa mara ya kwanza.

Kisha walikutana kwenye chakula cha jioni kabla ya nyota huyo wa Ureno kumuomba amchumbie.

Akizungumza kuhusu tarehe yake ya kwanza na Ronaldo, Rodriguez alianika kila kitu katika makala yake kwenye Netflix aliyoipa jina la "Mimi ni Georgina"

"Nilifurahi sana, na tukiwa njiani kuelekea mgahawani, mikono yetu iligongana, na nilihisi kana kwamba mikono hiyo ilikuwa nami kwa muda mrefu, na tulipogongana tena, tulishikana.

"Baada ya chakula cha jioni, nilienda nyumbani na moyo wangu ulikuwa unadunda kwa nguvu mno. Nilikuwa na furaha ya kipekee sana.

"Wakati wa kipekee zaidi ulikuwa Jumamosi. Nilikuwa natamani kumuona na kuwa naye, lakini sikutaka kumtumia ujumbe. Aliniandikia ujumbe baada ya mchezo na bila shaka, sikumwambia kwamba nilikuwa tayari kwa lolote, nikamwambia kwamba nilikuwa nimekaa nyumbani na kwamba nilikuwa nataka kulala.

"Akaniambia: 'unataka kula chakula cha jioni?' na nikasema: 'Sawa'. Nilikuwa tayari nimekula. Alikuja kunichukua nyumbani. Tukafika kwake. Nilifurahi mno kama kila mwanamke anapopata mwanaume wake."

Baada ya tarehe yao ya kwanza, Ronaldo alikuwa anakwenda kumchukua Rodriguez kazini kwenye gari lake la Bugatti kama anavyoeleza:

"Alikuwa anakuja kunichukua baada ya kazi. Kuna wakati alikuja na gari yake ya Bugatti. Wenzangu walikuwa wakinipiga picha. Nilifika kwa basi na kuondoka kwa Bugatti."

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid alielezea kuhusu kukutana kwake na Georgina kwa mara ya kwanza, akisema kwamba alimvutia mno.

"Tulipocheza kwa kiwango cha juu, ilikuwa wakati wa kipekee ... alikuwa msichana wa kuvutia, mkomavu, na nilianza kuhusishwa ... na uhusiano wa kupendeza sana. Baada ya muda, nilihisi kuwa yeye ndiye mwanamke wa maisha yangu."

Wapenzi hao wana watoto watano, watatu kutoka kwa mama wawili tofauti.

## ISIKUPITE

TANGU miaka 19 iliyopita hadi leo, Cristiano Ronaldo, alipocheza mechi yake ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ameweka rekodi ya; mfungaji wa mabao mengi zaidi (140), kinara wa kucheza mechi nyingi (183), kushinda mechi nyingi za fainali (5), mabao mengi kwa msimu (17) na nyingine ni mabao mengi kwenye hatua ya mtoano (67).



NIPASHE JUMATATU APRILI 17, 2023



# WACHEZAJI 5 WANAOFANANA KIUCHEZAJI NA LIONEL MESSI




**LONDON,** England

LIONEL Messi ndiye mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Tayari amewatia moyo wanasoka wa kizazi kipya na ataendelea kufanya hivyo kwa siku zijazo. Kumtazama Messi akikua kutoka winga mwembamba na mwenye miguu mahiri hadi mshindi wa dunia imekuwa tukio la kuridhisha na la kipekee.

**Ndio maana ulimwengu ulisherehekea pamoja alipoivusha Argentina na kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia Desemba 2022. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ni mmoja wa washambuliaji waliocheza vema wakati wote. Ustadi wake mzuri wa kucheza chenga huwaacha mabeki wanyonge huku uwezo wake wa ajabu wa kupiga mashuti ukiendelea kuwafanya walinda mlango kuwa na wakati mgumu.**

Ni kawaida kwa wanasoka kwenye mchezo wa leo kupata msukumo kutoka kwa Messi. Baada ya yote, mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or ni mmoja wa wanasoka wenye ushawishi mkubwa zaidi wa wakati wote.

Hapa tunawatazama wanasoka watano wenye uchezaji unaofanana na Messi, twende sasa...

**#5 Phil Foden (Manchester City)**

Phil Foden ni mmoja wa washambuliaji wachanga wanaosisimua zaidi ulimwenguni hivi sasa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ni zao la akademi ya Manchester City na tayari ni tegemeo katika Timu ya Taifa ya England.

Foden ni mchezaji anayetumia mguu wa kushoto ambaye anaweza kucheza katika nafasi kadhaa kwenye safu ya mbele na kiungo. Kama Messi, mpira unashikamana na miguu ya Foden na ni vigumu kumnyang'anya mpira. Pia ni mwanasoka mbunifu ambaye maono yake yanalingana na sifa zake za kiufundi.

Foden, kama vile Muargentina huyo mashuhuri, hafanyi mambo mengi ya kuvutia anapokuwa anamiliki mpira.

Pia, anafanya vema katika kucheza kama namba tisa kama alivyofanya nguli huyo wa Argentina katika siku zake za ujana chini ya kocha Pep Guardiola alipokuwa akiinoa Barcelona.

**#4 Paulo Dybala (AS Roma)**

Paulo Dybala ni mmoja wa washambuliaji wenye vipaji vya ufundi wa kizazi chake. Hata hivyo, wasifu wa Dybala unakaribia kufanana na wa Messi. 'La Joya' alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Juventus wakati wa kipindi cha mafanikio zaidi cha 'Bianconeri' katika muongo uliopita.

Dybala anaweza kucheza katika nafasi mbalimbali kama mshambuliaji wa kati, mshambuliaji wa pili, kiungo mkabaji, namba tisa au kama winga wa pembeni. Anasifika kwa ustadi wake wa kuchezea chenga na uwezo wa kupiga mashuti ambao unafanana sana na ule wa Messi.

**#3 Riyad Mahrez (Manchester City)**

Uchezaji wa Riyad Mahrez una sifa nzuri zaidi, yeye ni mshambuliaji ambaye mtindo wake wa uchezaji unafanana sana na wa Messi. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria kwa kawaida hucheza chini ya winga ya kulia na kuwapita mabeki kutokana na uwezo wake wa ajabu wa kupiga chenga.

Mshambuliaji huyo anapenda kukata kutoka ubavuni na kupiga mashuti kwa mguu wake wa kushoto wenye nguvu zaidi. Mahrez anaonesha uwiano mkubwa, kasi na ustadi kila anapopanda na mpira na anachukuliwa kuwa mmoja wa mawinga bora zaidi kwenye mchezo huo.

**#2 Neymar Jr (Paris Saint-Germain)**

Neymar Jr. ni mmoja wa marafiki wa karibu wa Lionel Messi katika soka. Wawili hao walishiriki uhusiano mzuri wakati walipokuwa pamoja Barcelona kati ya mwaka 2013 na 2017 na sasa wanaleta uharibifu pamoja wakiwa Paris Saint-Germain.

Kama mchezaji mbunifu, Neymar anafanana sana na mwenzake wa PSG kwa jinsi anavyocheza. Anafunga mabao na kutengeneza nafasi nyingi kwa wachezaji wenzake. Mbrazil huyo mara nyingi anakosolewa kwa matendo yake nje ya uwanja.

Lakini hiyo haibadilishi ukweli kwamba yeye ni mmoja wa washambuliaji bora wa zama za kisasa. Messi na Neymar ni wachezaji wawili wabunifu na stadi wa wakati wote.

**#1 Mohamed Salah (Liverpool)**

Mohamed Salah alijiunga na Liverpool msimu wa majira ya joto wa 2017 na akafanikiwa kuwa mshindi wa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa chini ya kocha Jurgen Klopp. Amekuwa mchezaji muhimu zaidi wa Liverpool katika miaka ya hivi karibuni. Salah ni mtambo wa kupachika mabao na uchezaji wake unafanana kabisa na wa Lionel Messi.

Miguu ya haraka ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri, mwendo wa kasi na wepesi vyote vinamfanya kufanana na nyota huyo wa Argentina. Pia amekuwa na kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa akiwa na Liverpool.

Salah amefunga mabao 173 na kutoa asisti 69 katika mechi 280 kwenye mashindano yote akiwa na Liverpool hadi sasa.

## Nukuu

"Nina uzoefu pale Palmeiras (ya Brazil) ilipokaa bila kutwaa ubingwa kwa miaka 20, hapa ni sawa kabisa. Ndio maana nimekuja, sisemi tutashinda ubingwa wa ligi kwa sababu hakuna kilichoamuliwa bado, lakini tupo pale. kupigana hadi mwisho," **Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus, akiionya klabu yake ya zamani, Manchester City kuhusu mbio za ubingwa Ligi Kuu England.**



"Kama nilivyosema katika mkutano na waandishi wa habari uliopita, ni kushinda, kushinda, kushinda. Wao [Arsenal] wamekuwa na mwendo wa kustaajabisha hadi sasa msimu huu, sidhani kama watapoteza pointi nyingi na lazima tuwe humo. Ni muhimu kwetu kufika kwenye mechi kwa kushinda leo (juzi) na [ni] fainali [dhidi ya Arsenal] katika mchezo ujao wa Ligi Kuu," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, baada ya juzi, Jumamosi kuichapa Leicester City mabao 3-1.**



"Rio Ferdinand na JT (John Terry) walikuwa na misimu mibaya katika maisha yao ya soka kama wachezaji wote, VVD (Van Dijk) ana moja tu. Hakuna beki wa kati katika enzi ya Ligi Kuu England aliyewahi kuwa na mchango mkubwa kwa timu kama Dijk," **Mlinzi wa Liverpool, Virgil van Dijk huenda hajawa kwenye kiwango bora msimu huu, lakini Jamie Carragher, anasema ndiye beki wa kati bora zaidi katika historia ya Ligi Kuu England.**



Nipashe
# Spotika



LIONEL Messi ndiye mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Tayari amewatia moyo wanasoka wa kizazi kipya na ataendelea kufanya hivyo kwa siku zijazo. Kumtazama Messi akikua kutoka winga mwembamba na mwenye miguu mahiri hadi mshindi wa dunia imekuwa tukio la kuridhisha na la kipekee.

Uk. 12&13



JEAN BALEKE

# MABAO 10 BORA ROBO FAINALI KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwangwo**

NI timu nne tu zimebaki kwenye Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), maarufu Kombe la FA, ikimaanisha kuwa imefikia hatua ya nusu fainali.

Timu hizo ni Mabingwa Watetezi Yanga, Simba, Azam na Singida Big Stars. Hatua ya robo fainali ilianza Aprili 2, Singida Big Stars ilipoibwaga Mbeya City mabao 4-1, kwenye Uwanja wa Liti, Singida kisha Aprili 3, Azam ikaishindilia Mtibwa Sugar mabao 2-0, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

**Aprili 7, Simba ikifanya mauaji kwenye Uwanja wa Azam Complex, ilipoirarua Ihefu mabao 5-1 na kutinga hatua ya nusu fainali, kabla ya Aprili 8, mwaka huu, Yanga kuondoka na ushindi wa bao 1-0 kwenye uwanja huo huo.**

Bingwa wa michuano hii huiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika. Jumla ya mabao 14 yamefungwa kwenye hatua hiyo ya robo fainali na kwenye makala haya tutayaangalia mabao 10-bora yaliyofungwa kwa ustadi kwenye hatua hiyo...

**#1. Rafael Daudi (Ihefu vs Simba)**

Wakati Simba iliongoza kwa mabao 4-0, dakika ya 60, Ihefu ilipata faulo pembeni kulia mwa lango, iliyokwenda kupigwa na Never Tigere.

Si mabeki wa Simba wala kipa wao Aishi Manula aliyekuwa akiuona ukija aliyehangaika kuruka zaidi ni Rafael Daudi ambaye alikwenda juu kidogo na kuupiga kichwa mpira ukajaa wavuni na kumwacha kipa na wachezaji wake wakilaumiana.

**#2. Saido Ntibazonkiza (Simba vs Ihefu)**

Kipa wa Ihefu, Shaaban Kado alimuanzia beki wake wa kushoto Yahaya Mbegu kushoto mwa uwanja. Saidi Ntibazonkiza alikuwa anakuja kwa kasi kukabia juu, hivyo kumfanya beki huyo kuteleza, na Mrundi huo akaupitia mpira, akavuta hatua mbili tu kabla ya kuachia fataki lililojaa ndani ya wavu dakika ya 39, likiwa ni bao la nne, Simba ikiondoka na ushindi wa mabao 5-1.

**#3. Bright Adjei (Singida Big Stars vs Mbeya City)**

Bright Adjei wa Singida United alifunga bao maridadi kwenye mechi kati ya timu yake dhidi ya Mbeya City iliyochezwa Uwanja wa Liti, Singida.

Ilikuwa ni dakika ya tisa alipopachika bao la pili akiunganisha krosi iliyochongwa na Dickson Kibabage, Kazadi akaukosa, ukamkuta mfungaji ambaye aliusukumizia wavuni.

**#4. Jean Baleke (Simba vs Ihefu)**

Ilikuwa ni dakika ya 15 ambapo Jean Baleke alipofunga bao lake la pili, kabla hajatimiza 'hat-trick' yake kwenye mechi dhidi ya Ihefu, alipoupata mpira wa pasi ndefu iliyopigwa na Kibu Denis, akakokota ndinga, na kiasi cha mita 20 hivi kutoka golini alichia kombora kali la mguu wa kushoto ukajaa wavuni, pembeni mwa kipa Shaaba Kado.

Ilikuwa ni kazi nzuri ya Kibu aliyemkwepa Peter Mwalyanzi aliyetaka kumsukuma, hivyo akaanguka na mwamuzi akaamuru mpira uendelee, akaondoka kwa kasi kabla ya kummegea mfungaji.

**#5. Fiston Mayele (Yanga vs Geita Gold)**

Mayele aliugusa tu mpira kupoteza uelekeo, kutokana na krosi ya Tuisila Kisinda. Mpira ulikuta unakatisha kwenye mstari wa goli la Geita Gold, kabla ya mfungaji kuugusa, ukajaa ndani ya kimia dakika ya 57, likiwa bao pekee kwenye mechi hiyo, Yanga ikishinda bao 1-0.

Bao lilitengenezwa upande wa kushoto kwa Kibwana Shomari, akapeleka kwa Salum Aboubakar 'Sure Boy', aliyemtamngulizia Tuisila akamzunguka beki mmoja wa timu pinzani kabla ya kutimua mbio na kupiga majalo.

**#6. Pape Sakho (Simba vs Ihefu)**

Chama aliuchukua mpira katikati ya uwanja, akiwa peke yake aliondoka kwa kasi, likiwa ni shambulizi la kustukiza, 'counter attack', akammegea mfugaji ambaye aliwazidi mbio mabeki wawili wa Ihefu kabla ya kuujaza mpira wavuni kwa mguu wa kushoto dakika ya nne ya nyongeza, likiwa ni bao la tano la mchezo.

**#7. Eliud Ambokile (Mbeya City vs Singida Big Stars)**

Pamoja na kupoteza kwa kufungwa mabao 4-1, Mbeya City ilipata bao kali la kufutia machozi lililofungwa na Eliud Ambokile dakika ya 54, kipindi ambacho Singida Big Stars ikiongoza kwa mabao 3-0. Alipachika bao kwa kuubetua mpira.

**#8. Kipre Junior (Azam vs Mtibwa Sugar)**

Krosi iliyopigwa na Ayoub Lyanga ilipigwa kichwa na Idris Mbombo, lakini haikwenda langoni, bali ulikatisha eneo la lango ikionekana ni kama krosi nyingine hivi. Kipre alikutana na mpira huo ukizagaa na akaukwamisha wavuni dakika ya 27, likiwa ni bao la kwanza kwenye mechi hiyo.

**#9. Abdul Selemani Sopu (Azam vs Mtibwa Sugar)**

Sopu alipenyezewa mpira wa Idris Mbombo, ukawa mrefu kidogo, kipa wa Mtibwa Sugar akawa anatoka kuuwahi, lakini mfungaji akafanikiwa kuufikia na kuudokoa, mpira ukajaa ndani ya wavu. Lilikuwa ni bao la pili dakika ya 73 ya mchezo.

**#10. Bruno Gomes (Singida Big Stars vs Mbeya City)**

Mchezaji huyu raia wa Brazil, Bruno, alipigiwa pasi ndefu kutoka nyuma, ikionekana mabeki wa Mbeya City wakiwa wamepanda mbele. Akachomoka kama kipanga, akauwahi na kukimbia nao, kipa akatokea kwa nia ya kulipunguza goli, alichofanya akamdanganya kama anapiga, alipotikisika, akamlamba chenga, akabaki na goli tupu, kabla ya kuusukumizia wavuni.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Erling Haaland, amebakiza mabao mawili tu kufikia rekodi ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu England iliyowekwa msimu wa 1993/94 na Andy Cole wa Newcastle United ya kucheka na nyavu mara 34, ambayo pia ilifikiwa msimu uliofuata wa 1994/95 na Alan Shearer wa Blackburn Rovers.



## HABARI DODOMA

## Serikali yaagiza mashamba ya shule kuzalisha chakula

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI mkoani Singida imeagiza mashamba yote ya shule katika msimu ujao wa kilimo yatumike kuzalisha mazao ya chakula na biashara ili wanafunzi wapate chakula cha kutosha na kuongeza ufaulu.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wa Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa (ALAT) uliofanyika wilayani Ikungi.

Alisema ili kuondoa tatizo la utoro wa wanafunzi shuleni kila shule iweke utaratibu wa kulima mashamba na kwamba kufanya hivyo kutaongeza upatikanaji wa chakula shuleni.

Dk.Fatma alisema shule nyingi za Mkoa wa Singida zina maeneo makubwa yanayofaa kilimo lakini yanatumika kuzalisha kiasi kidogo jambo ambalo linaongeza mzigo mkubwa kwa wazazi katika kuchangia chakula shuleni.

"Serikali imeleta madarasa iliyobaki ni sisi viongozi kuhakikisha wanafunzi wanahudhuria darasani, wazazi kuhakikisha wanawalisha wanafunzi, lakini litakuwa jambo jema watoto wetu wakaanza kuyatumia mashamba ya shule kuzalisha chakula chao wenyewe," alisema.

Aidha, aliwaagiza maofisa elimu mkoani hapa kuhakikisha wanatumia mbinu mbalimbali za kufundishia zikiwamo matumizi ya vijiti vya kuhesabia ili kuondoa tatizo la baadhi ya wanafunzi kushindwa kusoma, kuandika na kuhesabu.

"Inashangaza mfano Shule ya Msingi Kisasida iliyopo Manispaa ya Singida yenye wanafunzi zaidi ya 1,000 kati ya hao 139 hawajui kusoma na kuandika," alisema.

Hivyo aliwataka walimu kuwa na nia ya dhati katika kuondoa tatizo la kusoma, kuandika, kuhesabu shuleni kwani wazazi wanawategemea katika mabadiliko ya watoto wao.

Pia, aliwagiza wakurugenzi na wenyeviti wa halmashauri za wilaya kuhakikisha wanatumia sheria ndogo kuondoa tatizo la utoro shuleni ili kuinua viwango vya elimu.

# Mbunge ataka tume kuchunguza kushuka uzalishaji korosho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuunda tume huru ya kuchunguza kushuka kwa uzalishaji wa zao la korosho katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota aliyasema hayo wakati akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka 2023/24.

Alisema pamoja na jitihada za serikali za kuratibu upatikanaji wa pembejeo kuna mdondoko wa zao hilo.

"Napongeza serikali kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwekeza katika tasnia ya korosho, tumeona kwa miaka mitatu mfululizo, serikali ikitoa pembejeo bure kwa wakulima wa korosho, tunaendelea kuishukuru serikali."

"Mwaka huu kuna mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 340 ambayo imetolewa na nina matumaini pembejeo hizi zitafika kwa wakati na wakulima wa korosho watanufaika na pembejeo,"alisema Chikota.

Alisema pamoja na uwekezaji ulifanywa na serikali kwenye tasnia ya korosho bado kuna anguko la uzalishaji wa korosho nchini ambapo kwa kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2017/18, Tanzania ilifikisha uzalishaji wa tani 320,000.

"Lakini kwa masikitiko makubwa katika msimu uliopita uzalishaji umepungua hadi kufikia tani 160,000 pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa, ukiuliza Bodi ya Korosho hawana majibu ya uhakika na hata Taasisi ya Utafiti ya TARI Naliendele hawana majibu ya kutoshereza ya anguko kubwa na uzalishaji wa korosho,"alisema.

Alisisiza: "Haiwezekani mikoa ya uzalishaji wa korosho imeongezeka, serikali imefanya uwekezaji wa kutosha lakini uzalishaji unazidi kuwa mdogo."

Chikota alisema malengo ya Bodi ya Korosho Tanzania mwaka huu ilikuwa ni kufikisha tani 400,000 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni kufikisha tani 700,000 ifikapo mwaka 2025.

"Kwa anguko hili kuna kazi kubwa inayopaswa kufanywa ili kufikia malengo na shauri serikali kuunda tume hii huru yenye wataalamu kutoka nje ili kupata mawazo mapya,"alisema.

Aliomba watumie wataalamu wa nje na Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA) ili kuangalia mfumo wa uagiziaji na udhibiti wa pembejeo kwa kuangalia ubora wake.



. Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (aliyevaa skafu), akiangalia wanafunzi wa shule ya sekondari Miyuji, wakitumia mojawapo ya kompyuta walizosaidiwa na Vodacom Tanzania Foundation, ikiwa ni sehemu ya mradi wa uunganishwaji wa shule za sekondari unaolenga kuziunganisha shule 300 Tanzania, kwa kushirikiana na 'African Child Projects' na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Taasisi hiyo ilikabidhi kompyuta 15 na vifaa vingine vya TEHAMA vyenye thamani ya zaidi ya sh. milioni 48 kwa shule 9 za sekondari, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Uwapo wa chakula shuleni wapunguza utoro kwa wanafunzi

**Na Renatha Msungu** MANYONI

KAIMU Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Lydia Ntitu amesema uwepo wa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi katika maeneo mbalimbali kumesaidia kupunguza utoro na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Aliyasema hayo wakati akipokea chakula kutoka Shirika la Word Vison Tanzania, kwa ajili ya shule nane za msingi zilizopo kwenye mradi wa kilimatinde wilayani Manyoni, chenye thamani ya Sh.milioni 89.9.

Shule zilizokabidhiwa vyakula hivyo ni Shule ya Msingi Solya, Mankembo, Saranda, Makuru B, Sasajila, Makasuku, Hika na Shule ya Msingi Chibumagwa.

Ntitu alisema uwepo wa chakula shuleni ni moja ya ushawishi wa wanafunzi kuhudhuria darasani kwa sababu anakuwa na uhakika wa kula mchana lakini pia anakuwa na uwezo wa kusikiliza masomo darasani.

Kutokana na hilo alilishukuru Shirika la World Vision Tanzania, kwa kutoa chakula hicho ambacho kimesaidia kuziba pengo ambalo baadhi ya wazazi wengine walishindwa kuchangia fedha kama utaratibu ulivyowekwa.

"Kama tunavyofahamu mpango wa serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ni kuwasaidia wanafunzi kupata chakula shuleni, hivyo World Vision wamekuja wakati muafaka,"alisema Ntitu.

Hata hivyo aliwataka walimu wa shule kuhakikisha chakula hicho kinahifadhiwa vizuri ikiwamo kugawiwa kwa wakati wanafunzi pindi wanapokuwa shuleni kuendelea na masomo ya kila siku.

Mratibu wa wa mradi huo, Rukia Msuya alisema mradi huo unafanya kazi katika vijiji 17 vilivyopo kwenye kata tano zilizopo Wilaya ya Manyoni mkoani Singida.

Msuya alisema lengo la mradi huo ni kuboresha maisha ya mtoto, familia na jamii, akisema ndiyo maana shirika hilo linashirikiana na serikali ili kuhakikisha wanafunzi wanapata lishe mashuleni.

Alisema chakula walichotoa ni pamoja na mahindi, maharagwe, mafuta pamoja na chumvi ambazo zimetolewa katika shule nane zilizoanishwa kwa ajili ya kupata msaada huo.

Nelly Antony mmoja wa wanafunzi aliishukuru serikali kutokana na kuanzisha mpango wa kutoa chakula kwa wanafunzi shuleni, akisema umesaidia wanafunzi kuhudhuria darasani.



# Madereva wengi Mbeya hawajapata mafunzo, hawana vyeti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya madereva wa vyombo vya moto mkoani Mbeya wamebainika hawajawahi kupata mafunzo ya udereva kwenye vyuo vinavyotoa mafunzo hayo, hali ambayo inawafanya wakose weledi, kuhatarisha maisha yao na ya watumiaji wengine wa barabara.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ukaguzi wa magari ya abiria na binafsi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama.

Alisema kutokana na hali hiyo, jeshi hilo limeagiza madereva wote mkoani humo kupeleka vyeti vyao pamoja na leseni za udereva ili vihakikiwe.

Alisema uhakiki huo ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Camillus Wambura ambalo alilitoa hivi karibuni kwa makamanda wa polisi wa mikoa yote nchini.

Alisema madereva wote ambao watabainika kuwa hawajapita kwenye vyuo vya udereva watatakiwa kwenda ili waendane na matakwa ya sheria kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani ambazo baadhi zimekuwa zikitokana na kukosa weledi kwa madereva.

"Ni kweli unaweza ukawa mahiri sana kwenye uendeshaji wa gari lakini kama hujapita kwenye vyuo vinavyotoa mafunzo hiyo ni kazi bure, utaakiwa kwenda kupata mafunzo hayo kwenye vyuo vyetu vya ufundi stadi ama shule zinazofundisha udereva," alisema Kamanda Kuzaga.

Kwa upande wake Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Yusuph Kamota alisema kwa sasa ukaguzi huo unafanyika kwa hiyari ndani ya wiki mbili na baada ya hapo wataanza kuchukua hatua za kisheria. Alisema wataendesha operesheni maalumu ya kuwasaka madereva wasiokuwa na vyeti lakini wanaendesha magari na wana leseni ili wachukuliwe hatua za kisheria. Alisema watakagua magari yote yakiwemo ya abiria, ya watu binafsi pamoja na malori na kwamba ukaguzi huo wa hiyari utafikia ukomo mwishoni mwa Aprili mwaka huu na hivyo akawataka madereva kwenda wenyewe kukaguliwa.

"Tutaweka mkazo kwenye magari ya abiria ambayo yana leseni C, C1, C2, C3 na leseni E ambayo ni ya malori, tutakagua kila gari ambalo linapita barabarani na tutachukua hatua kali za kisheria," alisema Kamota.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Rajab Ghulika aliwataka madereva ambao hawajapita kwenye vyuo waende vyuoni ili wakapate umahili wa kufanya kazi hiyo.

Alisema hata ambao wana vyeti na walipata mafunzo miaka ya nyuma wanaruhusiwa kwenda vyuoni kupata mafunzo ili kujifunza alama na michoro mipya ya usalama barabarani pamoja na kujikumbusha vitu ambavyo wamesahau.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga (wa nne kulia), akishirikiana na wadau mbalimbali wa usalama barabarani mkoani humo, kukata utepe kuzindua ukaguzi wa vyeti vya madereva pamoja na magari mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Watakiwa kuchangamkia fursa maonyesho nane nane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wametakiwa kuchangamkia fursa ya maonyesho ya kimataifa ya kilimo ambayo yatafanyika mkoani humo mwaka huu kwa kuboresha huduma zao ili kuwavutia wageni.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu maandalizi ya maonyesho hayo ambapo alisema maonyesho hayo ni fursa kwa wananchi. Alisema wamiliki wa hoteli wanatakiwa wajiandae kupokea wageni wengi kwenye maeneo yao na hivyo ni muhimu wakaboresha zaidi huduma zao.

Alisema maandalizi yameshaanza ikiwa ni pamoja na vikao vya maandalizi, ukusanyaji wa michangho kutoka kwa wadau pamoja na waonyeshaji mbalimbali watakaoshiriki.

Vilevile alisema wanaendelea na maboresho ya miundombinu mbalimbali katika Uwanja wa John Mwakangale ambao ndio unatumika kwa maonyesho hayo.

Alisema miundombinu ambayo inaboreshwa ni barabara, majengo, miundombinu ya maji pamoja na umeme ili kuhakikisha shughuli hiyo inafanyika vizuri na kwa tija zaidi.

Aidh,a alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo inaendelea na maandalizi mbalimbali ya kuhakikisha hali ya amani inaimarika wakati wote.

# Siri ya ufaulu wanafunzi wa sekondari yatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

BIDII na kujituma kwenye masomo imetajwa kuwa ndiyo sababu ya baadhi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya sekondari kufanya vizuri na kufikia malengo yao.

Meneja Miradi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Masozi Nyirenda aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Isimila iliyopo mkoani Iringa ambako alikuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo.

Alisema kwa miaka ya karibuni, Shule ya Sekondari Isimila ni miongoni mwa shule zinazofanya vizuri ambapo matokeo ya miaka mitatu yameonesha hakuna mwanafunzi yeyote aliyepata daraja sifuri kwenye mitihani ya kitaifa. "Nimefurahishwa kuona namna uongozi wa shule hii unavyoendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha wanafunzi wake wanaendelea kupata matokeo mazuri, miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha miundombinu," alisema Nyirenda.

Alisema shule hiyo imeongeza vyumba vya madarasa vinne, ofisi mbili pamoja na kutengeneza madawati 130 ambapo alisema miradi hiyo imetekelezwa vizuri kutokana na kuwepo kwa ushirikiano mzuri kati ya serikali na uongozi wa shule hiyo.

Nyirenda alisema, TEA ilianzishwa kwa lengo la kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao unalenga kusaidia jitihada za serikali za kuongeza upatikanaji wa elimu bora na kwa usawa nchi nzima.

Kupitia mfuko huo, Sh. bilioni 1.1 zimetolewa katika kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya kufadhili sekta ya elimu mkoani Iringa.

Aidha, aliushauri uongozi wa shule kuwasilisha maombi ya ufadhili kwenye mamlaka hiyo kwa ajili ya kusaidia kukabiliana na upungufu wa miundombinu mingine shuleni hapo.

Aliwapongeza wahitimu wote wa kidato cha sita kwa hatua waliyofikia na kuwataka waendelee kufanya maandalizi kwa ajili ya mitihani yao ijayo ili wafanye vizuri na kuendeleza historia ya shule hiyo ya kutofalisha hata mwanafunzi mmoja.

Awali akitoa taarifa ya maendeleo ya shule hiyo, Mkuu wa Shule, Mwalimu Frank Mahenge alisema shule ina wanafunzi 1,178 kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita.

Alisema kati ya wanafunzi hao wasichana wapo 835 na wavulana 343, huku kidato cha tano na sita wakiwa ni wasichana pekee jambo ambalo linasababisha wasichana kuwa wengi zaidi.

Alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri kwenye mitihani ya mwisho ya Taifa na kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo 2020 - 2022 shule ilifaulisha wanafunzi kwa asilimia 100 hivyo kuwa moja ya shule zinazofanya vizuri.

Aliitaja baadhi ya miundombinu ambayo inahitajika kuwa ni pamoja na jengo la utawala, jengo la maktaba kwa ajili ya wanafunzi kujisomea pamoja na mashine za kudurufu mitihani shuleni hapo.

Katika risala yao, wahitimu wa kidato cha sita waliishukuru serikali kwa kuanzisha mfumo wa elimu bila malipo kwa maelezo kuwa imesaidia hata watoto wanaotoka kwenye familia duni kupata elimu.

Walisema mbali na elimu bila malipo pia serikali imekuwa ikijenga miundombinu ya elimu kwa ajili ya kuboresha mazingira ya wanafunzi hao kujifunzia.





# Mfumuko wa bei za bidhaa washuka Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KIWANGO cha mfumuko wa bei kwa kipindi cha Machi 2023, kimeshuka na kufikia asilimia 7.09 kutoka asilimia 7.77 kilichorekodiwa kipindi cha Februari mwaka huu.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Bei kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salma Saleh Ali, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kiwango cha mfumuko wa bei za chakula na vinywaji visivyo na vileo kilipungua hadi asilimia 10.06 kipindi cha Machi 2023 kulinganisha na asilimia 10.23 iliyorekodiwa kipindi cha Februari 2023.

Alisema faharisi za bei ziliongezeka hadi 104.31 mnamo Machi 2023 ikilinganishwa na 97.41 Machi mwaka jana.

Alizitaja bidhaa zilizochangia kushuka kwa kiwango cha mfumuko ni pamoja na mchele wa jasmin asilimia 0.8, unga wa ngano asilimia 3.4, unga wa sembe asilimia 0.5, ndizi za mtwike asilimia 16.7, sukari nyeupe asilimia 0.9, na mafuta ya dizeli asilimia 0.3.

Mchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Ulrick Mumburi, alisema, kushuka kwa mfumko kulichangiwa na kuendelea kuimarika kwa dola kwenye mzunguko wa fedha.

Hata hivyo, alisema bado hali ya kiuchumi iko vizuri kutokana na kuwepo kwenye tarakimu moja ambayo ndiyo njia bora ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza nchini.

Mchumi Mkufunzi Mwandamizi kutoka Shule ya Biashara, Dk.Estella Ngoma Hassan, alisema kushuka huko kwa kiwango cha mfumko ni hali ya kawaida kulingana na mwenendo wa kibiashara.

## Serikali yaanzisha kamati kusikiliza, kutatua migogoro ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, imeanzisha kamati ya kusikiliza malalamiko ya migogoro ya ardhi kutoka kwa wananchi, kuifanyika kazi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Maisara.

Alisema kamati hiyo inaongozwa na Waziri wa Wizara hiyo, Rahma Kassim Ali.

Aidha, alisema kuna kesi nyingi zinazopokelewa katika wizara hiyo ambapo awali walikuwa wakipokea chache lakini baadaye ziliongezeka hali iliyosababisha kutenga siku maalum ya kusikiliza kesi hizo.

"Mwanzo tulikuwa tunasikiliza kwa siku moja tu malalamiko ya migogoro ya ardhi lakini kadri siku zilivyokuwa zikisonga mbele basi migogoro ndiyo inaongezeka, tukaona tuweke siku mbili ambayo ni Alhamisi na Ijumaa," alisema.

Alisema kuwa kamati hiyo inasikiliza mgogoro na kutoa maamuzi, kesi inapokwenda wanasikilizwa na wanasheria pia watu wa pande zote mbili na kutakiwa kujaza fomu, huku wanasheria kwa kushirikiana na kamisheni ya ardhi watakwenda eneo husika kujiridhisha.

"Baadae wanaitwa pande zote mbili, ipo migogoro ambayo inaamulika hapa hapa wizarani na ipo mengine ambayo tunawapigia watu wa tasisi wanakuja na tunaiamua na migogoro mengine kwa uzito wake tunaipeleka mahakamani," alisema.

Alisema tangu kuanzishwa kamati hiyo kasi imekuwa kubwa na zaidi ya migogoro 170 imepokelewa, kati ya hiyo mingine imemalizwa kwa kupatiwa ufumbuzi, ipo iliyopelekwa mahakamani na mingine inaendelea kufanyiwa kazi.

Alibainisha kuwa kuna mwitikio mkubwa wa wananchi kuwasilisha malalamiko yao na wizara kupitia timu yake imejipanga vizuri kuhakikisha inapunguza migogoro ya ardhi nchini.

Hivyo, aliwaomba wananchi kuitumia kamati hiyo ili changamoto zao ziweze kufanyiwa kazi na lengo la serikali la kupunguza migogoro ya ardhi nchini liweze kufikiwa.



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Tigo, CPA Innocent Rwetabura (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Mohamed (katikati) katika hafla ya iftar iliyoandaliwa na Tigo Zanzibar mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mauzo wa Tigo, Uthman Madati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Meli iliyobeba watalii 400 yawasili Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MELI ya Seabourn Sojourn iliyobeba watalii 400 imewasili visiwani Zanzibar juzi ikitokea Marekani na Ulaya.

Meli hiyo iliwasili katika Bandari ya Malindi Mjini Unguja ambapo watalii hao walitembelea katika vivutio mbalimbali vya utalii kwa muda wa siku mbili na kuondoka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya kuwasili wa meli hiyo na kuwapokea watalii hao, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, alisema ujio wa wageni hao ni fursa ya nzuri ya kuitangaza Zanzibar.

Alisema ujio wa watalii hao pia itaongeza pato la serikali kupitia pesa za kigeni sambamba na kukua kwa sekta ya utalii nchini.

Alisema lengo la serikali ni kuibadilisha Bandari ya Malindi Zanzibar kwa ajili ya kupokea meli za aina hiyo mara kwa mara.

Waziri Simai alisema kuwa malengo ya wizara yake ifikapo mwaka 2027 ni kupokea angalau meli tano kwa mwezi kutoka nchi mbalimbali.

Naye kepteni wa meli hiyo, Kyriakos Karras, alisema wameanza safari yao kutoka jijini Miami Florida na kwenda sehemu mbalimbali ikiwemo visiwa vya Shelisheli na watakapoondoka Zanzibar watakwenda jijini Dar es salam na kumalizia Afrika ya Kusini.

Alisema alifurahishwa na huduma nzuri, mandhari na watu wakarimu wa Zanzibar kutokana na mapokezi waliyopokelewa.

Mkuu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Azana Hassan Msingiri, alisema watahakikisha wanaimarisha ulinzi ili wageni hao wawe salama wakati wote wakiwa Zanzibar.

# Watu milioni 11 mikoa mitatu kunufaika upandaji miti

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Morogoro, mkoani hapa kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), limeanza mkakati maalumu wa uhifadhi mazingira katika vyanzo vya maji kwenye mito tegemezi ambayo ndio chanzo cha maji kwa watu zaidi ya milioni 11 wa mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Chini ya mkakati huo maeneo ya vyanzo vya chemichemi hai zinazotiririsha maji na kujaza vijito na mito yatapandwa miti rafiki ikiwamo ya matunda, karafuu na mazao ya viungo ambayo inasaidia kutunza na kuhifadhi mazingira kwenye maeneo ya vyanzo vya maji.

Katika kutekeleza mpango huo WWF imetoa bure miche 20,000 ya miti ya karafuu kwa wakulima wanaolima kandokando ya mito hiyo pamoja na vyanzo maji ili waweze kupanda na kisha kujinufaisha kiuchumi huku wakiendelea kuvitunza.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa miche ya karafuu na mazao ya viungo iliyofanyika katika kata Kinole, Ofisa Programu wa Maendeleo Endelevu Afrika wa WWF, Happness Minja, alisema mradi huo utahusisha kata nne zinazopitiwa na mito hiyo muhimu kwaajili ya vyanzo vya maji.

Minja, alisema lengo kuu la mradi huo pamoja na utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji pia utakuza uchumi wa wakulima kupitia upandaji wa miti ya mazao ya viungo ikiwamo karafuu na matunda.

Alitaja maeneo yatakayopandwa miti hiyo ni pamoja na Mto Mbezi kijiji cha Bagilo kata ya Tegetero, wananchi wanaolima katika chanzo cha maji cha Mto Mfizigo kijiji cha Tandai na Kalundwa kata ya Kinole.

Wengine ni wanaolima pembezoni mwa mito katika kijiji cha Kiswira kata ya Konde na Mto Mtombozi kwa wananchi wa kijiji cha Mtombozi na Lusange kata ya Mtombozi, Halmashauri ya wilaya hiyo Morogoro.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya wilaya hiyo ya Morogoro, Chesco Lwaduka, alisema katika mkakati huo wa kutunza mazingira na vyanzo vya maji, halmashauri hiyo imefanya utafiti inahitaji miche 1,113,042 ya karafuu, mdalasini miche 12,155,578, pilipili manga miche 5,825,212 na Iliki miche 5,452,709 ili ipandwe.

Alisema kutokana na mahitaji hayo halmashauri hiyo inawalika wadau wengine wa maendeleo kujitokeza ili kutimiza azma ya kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji kwaajili ya vizazi vya sasa na vijavyo huku akilishukuru shirika la WWF kwa kujitolea miti hiyo ya viungo.

Mkuu wa Kidakio cha Ruvu kati kutoka Ofisi ya Bonde la Wami/Ruvu, Richard Mwasenga, alisema alisema faida ya kupanda miti hiyo pembezoni mwa vyanzo vya maji ni pamoja na kusaidia kingo za mito na mmomonyoko wa ardhi.

Akizindua upandaji wa miche hiyo, Katibu Tawala Msaidizi upande wa uchumi na uzalishaji, Dk. Rozalia Rwegasira, alisema athari za uharibifu wa mazingira katika Mkoa wa Morogoro zimeanza kujitokeza kutokana na baadhi ya maeneo kuanza kukosekana kwa mvua.

Dk. Rozalia alisema kutokana na athari hizo kuna kila sababu ya kupanda miti yenye faida kama mikarafuu kwaajili ya kutunza mazingira na kuhifadhi vyanzo vya maji na kuachana na miti isiyo na faida kwa wananchi.

"Mkoa umeweka mkakati wa kupanda miti yenye faida kama hii mikarafuu katika kuhifadhi mazingira kwakuwa anayepanda ataweza kuutunza na baadaye kupata mavuno na kujiinua kiuchumi tofauti na miaka ya nyuma tulikuwa tukipanda miti isiyo na faida na kuitelekeza" alisema, Dk Rozalia.




Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Alhad Omar (wa pili kushoto), akitoa msaada wa futari kwa watu wenye uhitaji katika eneo la Magomeni Mapipa, mkoani humo mwishoni mwa wiki. Wa (pili kulia) ni Mkurugenzi wa Lalji Foundation, Imtiaz Lalji. **PICHA: MARY GEOFREY**

## Viongozi wa dini waunga mkono Wabunge kupinga ushoga

**Na James Lanka,** MOSHI

VIONGOZI wa dini na wadau mbalimbali wa maendeleo mkoani Kilimanjaro wameunga mkono juhudi za Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania kupinga ndoa za jinsia moja, ushoga na usagaji.

Wakizungumza na waumini mbalimbali wa dini ya kiislamu pamoja na wananchi wengine walioshiriki katika futari maalumu iliyoandaliwa na Baraza la Kiislamu Tanzania (BAKWATA) mkoani hapa kwa watu wote katika viwanja vya ofisi za taasisi hiyo juzi, viongozi hao waliunga mkono wabunge hao ambao kwa pamoja walitaka kurekebishwa kwa sheria zinazounga mkono ndoa za jinsia moja, tabia za ushoga na usagaji.

Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mlewa Shabani, alifafanua kuwa hakuna mtu anayejua atakufa lini ndio maana kumetengwa muda wa mwezi mmoja kwa binadamu (Mwezi Mtukufu wa Ramadhani) kuzungumza na Mungu na kutubu dhambi zao na kutoa wito kwa Watanzania wote kuwaunga mkono wabunge wanaopinga mambo maovu yasiyompendeza Mungu ikiwamo ndoa za jinsia moja na tabia za ushoga na usagaji zinazorindima katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Tanzania.

"Binafsi kwa niaba ya Waislamu wa Mkoa wa Kilimanjaro, ninapenda kutumia nafasi hii kumpongeza mbunge wetu wa Moshi mjini, Priscus Tarimo kwa ushirikiano wake ambao amekuwa akiuonesha kwa viongozi wa dini mbalimbali ikiwemo sisi (Waislamu) pasipo ubaguzi wowote kwa maendeleo ya mkoa wetu na taifa kwa ujumla, tumuunge mkono kwa kupinga mambo yasiyofaa kama hili linalorindima kwa sasa la ndoa za jinsia moja," alisisitiza Shekhe Mlewa.

# Stanbic, UNDP kushirikiana upatikanaji mtaji maendeleo biashara

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic na Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo (UNDP) Tanzania, wametangaza ushirikiano wenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa mtaji na huduma za maendeleo ya biashara kwa kampuni changa na biashara ndogo na kati za kitanzania.

Ushirikiano huo, chini ya mipango yao ya Stanbic Biashara Incubator na Funguo Innovation Programme, unalenga kuboresha ubora wa huduma za maendeleo ya biashara zinazotolewa na watoa huduma tofauti na waendeshaji wa uvumbuzi kwa kampuni na biashara changa zinazoongozwa na vijana na wanawake.

Taarifa iliyotolewa na Stanbic na UNDP, imesema vilevile, mpango huo unalenga kukuza na kusaidia mazingira yatakayoruhusu kampuni hizo kustawi.

Kadhalika, ushirikiano huo unalenga kutoa mafunzo ya kiufundi na kujenga uhusiano na wawekezaji na wafadhili na kuongeza fursa kwa kampuni changa na biashara ndogo na kati ili kuongeza vyanzo mbalimbali vya mtaji.

Utiaji saini wa hati ya makubaliano, ulifanyika kwenye hafla fupi iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali wa ubunifu na ujasiriamali, kutoka sekta ya umma, binafsi, wadau wa maendeleo, waanzilishi wa kampuni za kibunifu pamoja na wandishi wa habari.

Kusainiwa kwa hati hiyo kuliashiria kuanza rasmi kwa ushirikiano huo na kuanza kwa shughuli ya kwanza ya pamoja, ambayo ilihusisha mafunzo ya siku mbili ya mbinu na maarifa ya kutafuta mitaji ya uwekezaji kwa kampuni changa na biashara ndogo na za kati.

Ushirikiano huo unaendana na lengo la 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, ambalo linasisitiza ushirikiano kwa maendeleo endelevu. UNDP Tanzania na Benki ya Stanbic Tanzania wanatambua kuwa ushirikiano ni muhimu katika kuendeleza mfumo wa uvumbuzi na ujasiriamali wa Kitanzania na wamejitolea kufanya kazi pamoja kukuza maendeleo endelevu kupitia ushirikiano.

Christine Musisi, Mwakilishi Mkazi wa UNDP Tanzania, alisema, "Tunafurahi kushirikiana na Benki ya Stanbic Tanzania kukuza ubunifu na ujasiriamali nchini Tanzania. Tunaamini ushirikiano huu utatusaidia kuongeza ufikiaji wa mtaji na huduma za maendeleo ya biashara kwa kampuni changa na biashara ndogo na kati za Kitanzania, hivyo kutengeneza fursa za ajira kwa vijana wa Kitanzania, na hatimae kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi."

Vivyo hivyo, Kevin Wingfield, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Stanbic Tanzania, alisema, "Tunafurahi kushirikiana na UNDP Tanzania kwenye mpango huu. Kama benki, tumejitolea kuunga mkono wajasiriamali na biashara ndogo ndogo, na tunaamini kuwa ushirikiano huu utasaidia sana kuongeza ufikiaji wa mtaji na huduma za maendeleo ya biashara kwa kampuni changa na biashara ndogo ndogo na kati za Kitanzania."



Moshi ukiwa umetanda katika anga la mji mkuu wa Sudan wa Khartoum baada ya kuzuka kwa mapigano kati ya kikosi cha wanamgambo cha RSF na wanajeshi wa serikali. **PICHA: AFP**

# Sudan kwawaka moto

- Mapigano makali yatanda Khartoum
- Ikulu yatekwa, rais hajulikani aliko

**KHARTOUM,** Sudan

MOTO unaendelea kuwaka nchini Sudan, baada ya kikosi Maalum cha Wanamgambo cha RSF, kusema kimechukua udhibiti kamili wa Ikulu ya rais, makazi ya Mkuu wa Jeshi, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan na uwanja wa ndege wa kimataifa wa Khartoum.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa hatua hiyo imechukuliwa katika kujibu mashambulizi yanayofanywa na jeshi dhidi ya kambi za RSF kusini mwa mji mkuu.

Awali kikosi cha RSF, kinachoongozwa na Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, anayefahamika zaidi kwa jina la Hemedti, kilisema kuwa jeshi lilizingira moja ya kambi zake na kufyatua risasi kwa kutumia silaha za kivita.

Wakati huo huo, vyama vya kiraia vya Sudan ambavyo vimesaini makubaliano ya awali ya kugawana madaraka na jeshi la nchi hiyo pamoja na kikosi cha RSF vimetoa wito wa kusitishwa kwa mapigano yaliyozuka baina ya vikosi hivyo viwili.

Kwa mujibu wa vyama hivyo, vimetoa wito kwa wadau wa kimataifa na kikanda kuchukua hatua haraka kuzuia umwagaji damu.

### BALOZI ZATAKA AMANI

Balozi wa Marekani nchini Sudan, John Godfrey, alijitokeza jana na kueleza kuongezeka kwa mivutano kati ya vikosi vya kijeshi nchini Sudan na kuibuka kwa mapigano, ni hali ya hatari.

Ametoa wito kwa uongozi wa juu kusitisha mapigano haraka.

Godfrey alisema wafanyakazi wa ubalozi wa Marekani, wamejihifadhi ndani ya ubalozi huo.

Aidha, ubalozi wa Russia nchini humo, ulisema una wasiwasi kutokana na kuongezeka kwa ghasia nchini humo na umetoa wito wa kusitishwa kwa mapigano na kufanyika mazungumzo.

Shirika la habari la Russia, (RIA) limeripoti juzi ubalozi huo ulisema hali katika mji wa Khartoum ni tete na inatia wasiwasi, lakini wanadiplomasia wa nchi hiyo wako salama.

Kwa upande wake Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken alisema hali nchini Sudan ni tete, lakini alisisitiza kwamba bado kuna fursa ya kukamilisha kipindi cha mpito kuelekea kuipata serikali inayoongozwa kiraia.

Misri nayo imeelezea wasiwasi wake mkubwa kutokana na mapigano yanayoendelea Sudan na imetoa wito kwa pande zote kujizuia.

### HOFU YA KIMATAIFA

Uingereza ilisema inafuatilia kwa karibu hali inayoendelea nchini Sudan na kwenye maeneo mengine ambako kuna mapigano ya kijeshi yanayoendelea.

Katika taarifa yake aliyochapisha Jumamosi kwenye ukurasa wake wa Twitter, ubalozi wa Uingereza pia uliwataka raia wake kubakia nyumbani na kufuatilia kwa karibu ushauri unaotolewa na ubalozi huo ikiwemo masuala ya safari.

Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, alivitolea wito vikosi vyote vinavyopambana nchini Sudan kuacha mapigano mara moja.

Borrell aliongeza kusema kuwa wafanyakazi wote wa Umoja wa Ulaya nchini Sudan wako salama.

Mkuu wa ujumbe wa amani wa Umoja wa Mataifa nchini humo (UNITAMS), Volker Perthes alitoa wito wa kukomeshwa mapigano yanayoendelea kati ya vikosi vya jeshi la serikali na wanamgambo.

Taarifa iliyotolewa na UNITAMS ilieleza kuwa Perthes analaani vikali kuzuka kwa mapigano nchini Sudan. "Perth amewasiliana na pande zote husika akiwarai wasitishe mara moja mapigano na kuhakikisha usalama kwa watu wa Sudan na kuliepusha taifa hilo na ghasia zaidi," ilieleza taarifa hiyo.

### WATU KADHAA WAUAWA

Taarifa iliyotolewa jana na muungano wa madaktari ilieleza kuwa raia watatu wameuawa na wengine kadhaa wamejeruhiwa wakati ambapo mapigano makali yanazidi kupamba moto baina ya vikosi vya kijeshi nchini Sudan.

Pande zote zinazohasimiana kila mmoja akimshutumu mwenzake kwa kuchochea ghasia.

Taarifa iliyotolewa na madaktari hao, ilisema kuwa raia wawili waliuawa katika uwanja wa ndege wa Khartoum, na mwingine mmoja aliuawa kwa kupigwa risasi kwenye jimbo la Kordofan Kaskazini.

Kwa mujibu wa kamati hiyo ya madaktari, watu wengine kadhaa wamejeruhiwa nchini Sudan, huku wengine wakiwa katika hali mbaya.

### NDEGE ZAAHIRISHWA

Huku hayo yakijiri shirika la ndege la Saudi Arabia, linalomilikiwa na serikali lilisema kuwa moja ya ndege zake aina ya Airbus, imepata ajali katika uwanja wa ndege wa Khartoum, kabla ya kuanza safari yake ya kuelekea Riyadh jana.

Taarifa hiyo haikutoa maelezo zaidi.

Saudia pia ilisema katika taarifa yake kuwa safari za ndege zake kwenda na kutoka Sudan zimesitishwa hadi hapo itakapotangazwa tena.

Nalo shirika la ndege la Misri la EgyptAir ,limesitisha safari zake za ndege kuelekea na kutoka Khartoum kwa muda wa saa 72 kutokana na mapigano hayo ya kijeshi katika mji mkuu, Khartoum.

Shirika la habari la Associated Press limeripoti kuwa ndege nyingine ya Ukraine ilionekana ikiwaka moto kutokana na mapigano hayo. **DW**

## Mwanasiasa auawa akiwa mubashara kwenye runinga

**MOMBAY,** India

MWANASIASA wa zamani wa India, ambaye alipatikana na hatia ya utekaji nyara, ameuawa kwa kupigwa risasi katika tukio lililorushwa mubashara katika runinga.

Atiq Ahmed, ambaye alikuwa chini ya usalama wa maofisa wa polisi, alikuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati bunduki ilipotolewa karibu na kichwa chake katika eneo la Prayagraj.

Baada ya risasi hizo kufyatuliwa, wanaume watatu waliokuwa wakijifanya wanahabari walijisalimisha haraka na kuwekwa chini ya ulinzi.

Mtoto wa kiume wa Ahmed, pia aliuawa kwa kupigwa risasi na polisi siku za nyuma. Makumi ya kesi, ikiwa ni pamoja na utekaji nyara, mauaji na unyang'anyi, zilisajiliwa dhidi ya Atiq Ahmed katika kipindi cha miongo miwili iliyopita.

Mahakama ya eneo hilo ilimhukumu yeye na wengine wawili kifungo cha maisha Machi mwaka huu, katika kesi ya utekaji nyara.

Ahmed alidai hapo awali kuwa kulikuwa na tishio kwa maisha yake kutoka kwa polisi. Video ilionyesha Ahmed na kaka yake, Ashraf, wote wakiwa na pingu, wakizungumza na waandishi wa habari wakiwa njiani kwenda kuchunguzwa afya zao hospitalini,sekunde chache kabla ya wote wawili kupigwa risasi.

Katika video hiyo, iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii na vituo vya televisheni, Ahmed alikuwa akiulizwa ikiwa alihudhuria mazishi ya mwanawe. **BBC**

HABARI MICHEZO

# MASHABIKI MTOKO WA KIBINGWA WALIVYOISHUHUDIA DABI KIBABE

Na Mwandishi Wetu

ACHANA na matokeo ya dabi ya jana, kule kwenye 'Betika Mtoko wa Kibingwa' ilikuwa ni hakuna mbambamba, kwa mashabiki 100 wa Simba na Yanga kuishuhudia dabi hiyo kwa staili ya kipekee.

Mashabiki hao ambao ni mabingwa wa Promosheni ya Betika Mtoko wa Kibingwa kwa siku mbili wamekuwa na matukio tofauti jijini Dar es Salaam yaliyokuwa na kaulimbiu ya hakuna mbambamba walipoanza kusherehekea 'bata' la msimu lililokuwa mahusuri kwa ajili ya kuisubiri mechi ya dabi ya watani wa jadi, Simba na Yanga iliyochezwa jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kabla ya mechi hiyo, Mabingwa hao kutoka mikoa mbalimbali nchini, walianza kwa kusherehekea bata la msimu huku wakitambiana kila upande ukijinasibu kuondoka na pointi tatu kwenye mechi hiyo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mabingwa kutoka mikoani, waliwasili Dar es Salaam kwa nyakati tofauti Jumamosi asubuhi na Ijumaa usiku kwa ndege na kuungana na wale wa Dar es Salaam jioni katika pati ya bata la msimu iliyofanyika Kidimbwi ikinogeshwa na msanii maarufu, Christian Bella, Dj d Ommy, Mussa Husein, Ibra Kasuga na Abby Chams.**

Kampuni ya Betika Tanzania imewagharamia mabingwa hao 100 ambao walishinda Promosheni ya Mtoko wa Kibingwa kuishuhudia dabi hiyo kwa hadhi ya VIP, huku juzi wakishiriki hafla hiyo iliyokwenda sanjari na burudani mbalimbali.

Sherehe hiyo ilifanyika kwa saa nne kuanzia saa 2:00 usiku hadi saa 6:00 ikiwa na burudani ya muziki, mashabiki wa pande zote mbili kutambiana na wachambuzi kuichambua dabi hiyo na burudani nyingine na jana Jumapili waliungana na maelfu ya mashabiki kuishuhudia dabi hiyo laivu pale kwa Mkapa.

Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Juvelinaus Rugambwa, alisema mabingwa hao wataondoka leo kwa ndege kurejea makwao.

"Betika hatuna mbambamba, mabingwa wetu 100 kama tulivyoahidi wameishuhudia dabi hii kwa hadhi ya VIP.

"Hii ni mara ya tano kwa Betika kuleta mabingwa wa Promosheni ya Mtoko wa Kibingwa kushuhudia dabi hiyo laivu huku kila msimu dadi ikiongezeka na safari hii ni mara mbili ya ile ya awali.

"Tukisema Mtoko wa Kibingwa, maana yake ni hii, imekuwa ni bandika bandua kwa washindi wetu ambao walipokelewa kibingwa Ijumaa na Jumamosi na kufikia kwenye hoteli ya nyota tano," alisema na kuongeza:

"Jumamosi kama ratiba ilivyokuwa imepangwa, walishiriki kwenye bata la msimu na kulala kwenye hoteli ya nyota tano na Jumapili (jana), waliishuhudia dabi laivu kwa Mkapa."

CHUMA HICHO...



Winga wa Simba, Denis Kibu, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Yanga iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Ligi ya Wanawake Daraja la Kwanza yapamba moto

Na Adam Fungamwango

LIGI Daraja la Kwanza Tanzania Bara kwa mchezo wa soka wanawake iliyoanza Jumamosi asubuhi jijini Mwanza, imeanza kupamba moto baada ya timu kuonyesha umwamba zikiisaka nafasi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Ligi hiyo inachezwa kwenye viwanja vya Nyamagana na CCM Kirumba asubuhi na jioni, ikishirikisha jumla ya timu 14 ambazo zimepangwa kwenye makundi manne.

Matokeo ya mechi hizo, Bunda Queens ilianza vema michuano hiyo kwa kuisasambua Masala Queens mabao 5-0 kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mapinduzi Queens ikiisulubu Lengo Queens 3-1, Singida Warriors ikiangukia pua kwa kuchapwa mabao 3-2 dhidi ya Ukerewe Queens, Bilo FC ikiikung'uta TSC Queens mabao 3-2, CCM Kirumba, halafu ikashinda mechi nyingine bao 1-0 dhidi ya Ukerewe Queens, huku Oysterbay Queens ikitoa kipigo cha mabao 7-0 dhidi ya MT Hannang Queens.

Baada ya raundi mbili, msimamo wa makundi yote inaonyesha Kundi A, Bunda Queens ya Mara, inaongoza ikiwa na pointi sita ikifuatiwa na Mapinduzi Queens ya Njombe ikiwa na pointi tatu, huku Kundi B likiongozwa na JMK Park Queens ya Dar es Salaam ikiwa na pointi sita.

Kundi C linaongozwa na Bilo FC ya Mwanza yenye pointi sita, ikifuatiwa na Ukerewe Queens pia ya Mwanza, yenye pointi tatu, na Kundi D kinara ni Oysterbay Queens ya Dar es Salaam yenye pointi tatu, ya pili ni Geila Gold ya Geita ambayo pia ina pointi tatu, ikizidiwa mabao tu ya kufunga na vinara.

# Kitayosce, Pamba zavutana, JKT Tanzania bado mbili

Na Adam Fungamwango

NI wazi Maafande wa JKT Tanzania wanasubiri muda tu kutangazwa kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara, kwani wanahitaji pointi mbili tu katika mechi tatu walizosaliwa nazo kwenye ligi ya Championship kuweza kupanda.

Timu hiyo juzi ilipata ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga dhidi ya African Sports na kufikisha jumla ya pointi 62, ikiendelea kuongoza kwa mbali kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kwa sasa inajitaji kushinda mechi moja, au kutoa sare mbili kati ya hizo tatu ili kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushuka msimu wa 2020/21.

Iwapo itashinda mechi yoyote kati ya tatu ilizosaliwa nazo, itafikisha pointi 65 ambazo haziwezi kufikiwa na Pamba yenye alama 51 iliyo kwenye nafasi ya pili au Kitayosce iliyo nafasi ya tatu.

Pamba kama itashinda mechi zote nne ilizosaliwa nazo itafikisha pointi 63 na Kitayosce ambayo nayo imesaliwa na mechi nne, itamaliza ikiwa na pointi 62 tu.

Katika hali inayoonyesha kuwa kuna mchuano mkali kupata timu ya pili itakayopanda moja kwa moja pamoja na JKT Tanzania, timu ya Pamba imepindua kibao baada ya kuiengua Kitayosce kwenye nafasi ya pili iliyoishikilia kwa muda mrefu, kwa kuichapa Mashujaa FC mabao 2-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Pamba imefikisha pointi 51 na kuitupa Kitayosce nafasi ya tatu kwa pointi zake 50, zote zikiwa zimesaliwa na michezo minne.

Pamba mabingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1990, iliteremka daraja mwaka 1999, na kwa misimu ya hivi karibuni imekuwa ikikwamia kwenye hatua ya mchujo, hivyo safari hii imepania kupanda moja kwa moja.

Msimu wa 2021/22 ilishindwa kutinga Ligi Kuu ilipotoka sare ya mabao 2-2 nyumbani dhidi ya Coastal Union na kuchapwa mabao 3-1 ugenini.

Timu mbili za juu kwenye ligi ya Championship zitapanda moja kwa moja, huku ya tatu na nne zitakwenda kucheza 'play off' na timu zitakazomaliza nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAXIMIN KUUZWA

KLABU ya Newcastle United haitampa winga Mfaransa, Allan Saint-Maximin, 26, mkataba mpya na itasikiliza ofa ya kumuuza. ***(Team Talk)***

### JUDE NA MAN CITY

MANCHESTER City ipo katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, 19, kutoka Borussia Dortmund msimu huu, lakini wanataka kuhakikishiwa kwamba anataka kufanya kazi na kocha, Pep Guardiola. ***(Mirror on Sunday)***

### ALLISTER ATAKIWA

KLABU ya Brighton inamthaminisha kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister, 24, kwa pauni milioni 60 hadi 70, lakini wanatumaini wanaweza kupata zaidi huku Chelsea, Liverpool na Manchester United wakimtaka mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### TCHOUAMENI HAUZWI

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Aurelien Tchouameni, 23, hana nafasi katika kikosi cha kwanza cha Real Madrid, lakini hawatasikiliza ofa ya kumuuza. ***(AS)***

### GAVI NI WA BARCA TU

KOCHA wa Barcelona, Xavi, hafikirii kiungo wa kati wa Hispania, Gavi, 18, atakuwa na furaha katika klabu tofauti baada ya kuhusishwa na na kuhamia Chelsea. ***(90min)***

### KESSIE, BROZOVIC KUPISHANA

BARCELONA na Inter Milan zimejadili mkataba wa kubadilishana unaomhusisha kiungo wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, 26, na kumuacha kiungo wa kati wa klabu ya Hispania na Croatia, Marcelo Brozovic, 30, kuelekea upande wa pili. ***(Gazzetta dello Sport)***

### COLWILL LULU CHELESEA

CHELSEA haina nia ya kumuuza beki wa Timu ya Taifa ya England chini ya miaka 21, Levi Colwill, 20, ambaye yuko kwa mkopo Brighton. Mchezaji huyo atakuwa sehemu ya kikosi cha kwanza cha Stamford Bridge msimu ujao. ***(Independent)***

### DIER MKATABA MPYA

KLABU ya Tottenham imeanza mazungumzo na mlinzi wa England, Eric Dier, 29, kuhusu mkataba mpya wa miaka mitatu hadi 2026 na wanataka ukamilike haraka bila kujali nani atakuwa kocha ajaye. ***(Football Insider)***


### SABITZER BADO HAKIELEWEKI

NAFASI ya kiungo wa Austria, Marcel Sabitzer, 29, kuhamia Manchester United kwa mkataba wa kudumu inategemea Bayern Munich iwapo itapunguza bei yao ya pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo. ***(Sun)***

### RB LEIPZIG YAIGUSA ARSENAL

KLABU ya RB Leipzig inavutiwa na mshambuliaji wa Arsenal, Folarin Balogun, 21, ambaye anawika kwa mkopo Reims kama mbadala wa fowadi wa Ufaransa, Christopher Nkunku, 25, ambaye anatazamiwa kujiunga na Chelsea msimu wa majira ya joto. ***(Todofichajes)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND AZIDI KUWEKA REKODI LIGI KUU ENGLAND

**●●● Tayari ameifikia rekodi ya Salah ya mabao 32, sasa aitafuta ya Cole na Shearer msimu...**

**MANCHESTER,** England

ERLING Haaland alifuga mabao mawili na kuifikia rekodi ya Mohamed Salah ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja katika ushindi wa 3-1 wa Manchester City dhidi ya Leicester City, Jumamosi.

**Haaland alifikisha mabao 32 na kuifikia rekodi ya Salah aliyefunga mabao hayo kwenye mechi 38 za Ligi Kuu England.**

Sasa Haaland, amebakiza mabao mawili tu kufikia rekodi ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu England iliyowekwa msimu wa 1993/94 na Andy Cole wa Newcastle United ya kucheka na nyavu mara 34, ambayo pia ilifikiwa msimu uliofuata wa 1994/95 na Alan Shearer wa Blackburn Rovers. Wawili hao waliweka rekodi hiyo baada ya mechi 42 za msimu wakati huo ligi hiyo ikijumuisha timu 22.

Siku nne tu mapema, Haaland alikua mchezaji wa kwanza katika soka la England kufunga mabao 45 katika msimu mmoja kwenye mashindano yote wakati wa ushindi wa 3-0 wa City dhidi ya Bayern Munich katika mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Jumamosi aliongeza rekodi hiyo hadi kufikia mabao 47.

Kocha Pep Guardiola alimtoa mshambuliaji huyo kipindi cha pili katika Uwanja wa Etihad Jumamosi, na kumpa mapumziko kabla ya mechi ya mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern.

Kikosi cha Guardiola, ambacho hakijafungwa katika mechi 14 za michuano yote, kimepitwa pointi tatu na vinara Arsenal wakiwa na mchezo mkononi katika mbio zao za mwisho za kuwania taji la Ligi Kuu England.

"Nadhani tumefurahishwa sana na pointi tatu zaidi. Pointi tatu zaidi karibu na Arsenal na tunawawinda," alisema kiungo wa kati wa Manchester, Kalvin Phillips akiiambia BBC.

"Viwango vyetu vilishuka kidogo kuelekea mwisho, kulikuwa na makosa machache na tulikuwa na mabadiliko kadhaa. Kwa ujumla tuna furaha na dakika 60 za kwanza au zaidi."

John Stones alianza kuifungia City katika dakika ya tano na Haaland alifanya matokeo kuwa 2-0 kwa penalti dakika ya 12, iliyotolewa kutokana na mpira wa mkono wa Wilfred Ndidi.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 553,

MECHI KALI

LEEDS
VERSUS
LIVERPOOL

1 | 4.03
X | 3.83
2 | 1.72

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MBAPPE ANAVUNJA REKODI YA PSG




**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amekuwa mfungaji bora wa muda wote wa Paris Saint-Germain kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, huku mabingwa hao wa Ufaransa wakipiga hatua kubwa kuelekea kulitwaa taji kwa ushindi wa 3-1 dhidi ya Lens wanaoshika nafasi ya pili kwenye Uwanja wa Parc des Princes Jumamosi.

Mbappe, ambaye tayari ni mfungaji bora wa PSG katika michuano yote, alifunga bao lake la 139 katika Ligue 1 dakika ya 31 na kumpiku Edinson Cavani.

Kufikia hatua hiyo, Lens tayari ilikuwa imepunguzwa hadi wachezaji 10 baada ya kadi nyekundu ya dakika ya 19 kwa Salis Abdul Samed kwa kumchezea vibaya Achraf Hakimi.

Wenyeji walijihakikishia ushindi kabla ya muda wa mapumziko kutokana na mabao zaidi ya Vitinha na Lionel Messi.

Vichapo vya mfululizo vya hivi majuzi kwa PSG vimeifanya Lens iliyo katika kiwango chake kufunga pengo kileleni mwa Ligue 1 hadi pointi sita pekee.

Lakini vijana wa Christophe Galtier walifanya kazi nyepesi kwa wapinzani wao Jumamosi kuongeza faida yao hadi alama tisa huku kukiwa na mechi saba za msimu kumalizika.



## *Lampard awashutumu wachezaji*

**LONDON,** England

KOCHA wa muda wa Chelsea, Frank Lampard aliikosoa timu yake kutopambana na kusema kwamba inabidi abadilishe hali ya klabu hiyo haraka kabla ya mechi dhidi ya Real Madrid Jumanne.

Lampard akizungumza baada ya kupoteza kwa mabao 2-1 katika Ligi Kuu England dhidi ya Brighton & Hove Albion, alisema Chelsea -- washindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ya mwaka 2021, ambao sasa wamekwama katika nafasi ya 11 kwenye Ligi Kuu, walikuwa wakionesha kushindwa kutimiza mambo ya msingi.

"Inasikitisha kwa kila ngazi," aliiambia Sky Sports. "Timu bora ilishinda na ingeweza kushinda kwa zaidi. Walicheza kama timu. Wanafanya kazi pamoja kwa muda mrefu.

"Lakini haitoshi kwa mtazamo wetu. Sehemu zote za msingi za soka -- kupigana, kukimbia, na mambo hayo -- tulikuwa na upungufu. Inabidi tujichimbue kwa haraka sana.

"Tuna mchezo mkubwa Jumanne. Hakuna haja ya kuwa chini sana, lakini kitaalamu tunapaswa kuelewa ni kwa nini leo ilienda jinsi ilivyokuwa. Na haikuwa nzuri kwelu."

Chelsea wamepoteza michezo yote mitatu tangu Frank Lampard arejee kama kocha wa muda.

# 549,430 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/04/23 | 17:00 | Istanbulspor vs Antalyaspor | 2.73 | 3.31 | 2.40 |
| 02. 19/04/23 | 17:00 | Kayserispor vs Kasimpasa | 2.31 | 3.35 | 2.83 |
| 03. 19/04/23 | 18:00 | Fotbal Trinec vs Pribram | 2.68 | 3.09 | 2.42 |
| 04. 19/04/23 | 20:30 | Konyaspor vs Adana Demirspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 05. 19/04/23 | 21:45 | Blackburn vs Coventry | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 19/04/23 | 21:45 | Swansea vs Preston | 2.44 | 3.16 | 2.76 |
| 07. 19/04/23 | 22:00 | Bayern Munchen vs Manchester City | 2.54 | 3.41 | 2.48 |
| 08. 20/04/23 | 20:30 | Sivasspor vs Trabzonspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 09. 20/04/23 | 22:00 | Sporting Lisbon vs Juventus | 2.34 | 3.17 | 2.97 |
| 10. 21/04/23 | 01:00 | San Lorenzo vs Fortaleza CE | 2.21 | 3.17 | 3.43 |
| 11. 21/04/23 | 05:00 | Universitario vs Goias | 2.23 | 3.12 | 3.01 |
| 12. 21/04/23 | 05:00 | Deportes Tolima vs CA Tigre | 2.27 | 3.28 | 3.17 |
| 13. 21/04/23 | 19:00 | Apollon Limassol vs Pafos FC | 2.44 | 3.27 | 2.74 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 17/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5014 | SQC Binh Dinh vs TT Ha Noi | 3.59 | 3.23 | 1.92 |
| 15:00 | 1421 | Argesul Pitesti vs Chindia Targoviste | 3.24 | 2.92 | 2.28 |
| 15:00 | 1496 | Van Yerevan vs Artsakh | 2.00 | 3.16 | 3.52 |
| 15:15 | 5478 | Hai Phong vs CLB Viettel | 1.89 | 3.39 | 3.49 |
| 16:00 | 5589 | Bandirmaspor vs Sakaryaspor | 2.30 | 3.24 | 2.72 |
| 16:00 | 5741 | Burnley U23 vs Bristol City U23 | 2.69 | 3.99 | 2.09 |
| 16:10 | 4280 | Bunyodkor vs Nasaf Qarshi | 3.25 | 3.05 | 2.00 |
| 17:00 | 2587 | CD Mafra U23 vs Sporting CP U23 | 3.36 | 3.72 | 1.87 |
| 17:30 | 2542 | NK Dubrava vs Orijent Rijeka | 2.12 | 3.29 | 2.99 |
| 18:00 | 4229 | Pyunik Yerevan vs Alashkert Martuni | 1.94 | 3.21 | 3.68 |
| 18:30 | 3340 | Bassam vs Denguele Sport | 3.72 | 2.94 | 2.04 |
| 19:00 | 1810 | Viking FK 2 vs Vidar | 1.98 | 3.99 | 2.81 |
| 19:00 | 2454 | Paide Linnameeskond vs FC Nomme United | 6.17 | 5.75 | 1.36 |
| 19:00 | 3289 | Sandecja vs Puszcza Niepolomice | 2.36 | 3.08 | 2.77 |
| 19:00 | 4435 | FCI Levadia Tallinn U21 vs Flora II | 1.74 | 4.16 | 3.94 |
| 19:15 | 4693 | KKS 1925 Kalisz vs Znicz Pruszkow | 2.01 | 3.37 | 3.27 |
| 19:30 | 1368 | Orleans vs FC Martigues | 2.31 | 2.94 | 3.20 |
| 20:00 | 2838 | Randers vs Nordsjalland | 3.30 | 3.51 | 2.05 |
| 20:00 | 3964 | West Bromwich U23 vs Sunderland U23 | 1.57 | 4.10 | 3.90 |
| 20:00 | 4265 | Stal Mielec vs Miedz Legnica | 2.21 | 3.12 | 2.97 |
| 20:00 | 4609 | Trelleborgs FF vs Orgryte IS | 2.26 | 3.36 | 3.04 |
| 20:00 | 4820 | Viktoria Koln vs Duisburg | 2.06 | 3.39 | 3.33 |
| 20:00 | 4834 | Jonkopings Sodra vs Gefle IF | 2.12 | 3.30 | 3.40 |
| 20:00 | 4868 | Honefoss vs Raufoss IL 2 | 1.26 | 5.94 | 6.76 |
| 20:00 | 5299 | Eik-Tonsberg vs Start 2 | 1.42 | 4.83 | 5.04 |
| 20:00 | 5822 | Varbergs Bois vs Sirius FK | 2.68 | 3.14 | 2.39 |
| 20:10 | 2225 | IFK Goteborg vs Malmo | 4.13 | 3.40 | 1.74 |
| 20:30 | 2307 | Nancy vs Red Star | 2.67 | 3.09 | 2.59 |
| 20:30 | 2707 | Genclerbirligi vs Altay | 1.83 | 3.50 | 3.60 |
| 20:30 | 2954 | Boluspor vs Caykur Rizespor | 3.33 | 3.38 | 1.95 |
| 20:30 | 3925 | Steaua Bucuresti vs Farul Constanta | 1.96 | 3.30 | 3.61 |
| 21:00 | 2034 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Utrecht | 1.95 | 3.54 | 3.34 |
| 21:00 | 3844 | FC San Pedro vs Club Omnisports de Korhogo | 1.82 | 3.22 | 4.16 |
| 21:00 | 5157 | Jong Ajax vs Jong PSV | 2.04 | 3.49 | 3.13 |
| 21:30 | 3517 | Al Fehaheel vs AL Arabi | 3.55 | 3.35 | 1.78 |
| 21:30 | 4259 | Al Salmiyah vs Kazma SC | 2.95 | 3.15 | 2.06 |
| 21:30 | 4310 | CA Fenix vs Canuelas | 2.58 | 2.86 | 2.76 |
| 21:45 | 2399 | Truro City vs Bracknell Town | 2.23 | 3.57 | 2.69 |
| 21:45 | 3893 | Fiorentina vs Atalanta | 2.29 | 3.25 | 2.90 |
| 21:45 | 4570 | Qalali vs Busaiteen | 4.10 | 3.30 | 1.69 |
| 21:45 | 5565 | Grenoble Foot vs St Etienne | 3.31 | 3.16 | 2.12 |
| 22:00 | 1133 | Levante vs Mirandes | 1.54 | 3.84 | 5.59 |
| 22:00 | 2718 | Vaca Diez vs Club Atletico Palmaflor | 3.31 | 3.57 | 1.93 |
| 22:00 | 2844 | Leeds vs Liverpool | 4.03 | 3.83 | 1.72 |
| 22:00 | 3500 | Celta Vigo vs Mallorca | 1.77 | 3.21 | 4.71 |
| 22:15 | 2282 | Vilafranquense vs CF Estrela | 2.39 | 3.18 | 2.76 |
| 22:15 | 2731 | FC Vizela vs Boavista | 1.85 | 3.37 | 4.03 |
| 22:15 | 5288 | Smouha Club vs Al Ahly Cairo | 6.26 | 3.99 | 1.48 |
| 22:30 | 1577 | CA Platense vs Colon Santa Fe | 2.23 | 3.01 | 3.12 |
| 22:30 | 3482 | Santiago Morning vs Cobreloa | 2.44 | 3.00 | 2.80 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SINGIDA BS: HATUTARUHUSU GOMES KUTUA YANGA SC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Singida Big Stars umesema hauna mpango wa kumuuza wala kumuachia kiungo wao mkabaji, Bruno Gomes, ambaye anahusishwa na kutakiwa na Yanga kuelekea dirisha kubwa la usajili.

**Hivi karibuni kulikuwa na taarifa kuwa uongozi wa Yanga uko katika mchakato wa kuhitaji huduma ya kiungo huyo kwa ajili ya usajili wa dirisha kubwa la msimu ujao wa mashindano.**

Hatua hiyo ni baada ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, kudaiwa kupendekeza jina la kiungo huyo ambaye amekuwa na kiwango kizuri na kusaidia Singida Big Stars katika michezo mbalimbali ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Singida Big Stars, Ibrahim Mirambo, alisema bado wapo na mipango na mchezaji huyo kwa ajili ya msimu ujao wa michuano iliyopo mbele yao.

Alisema hawana mpango wa kumuuza nyota huyo kwa klabu yoyote na kwamba wanachohitaji ni kukiimarisha kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu ujao ambao wanauhakika wa kushiriki michuano ya kimataifa.

Aliongeza kuwa, Bruno bado ana mkataba wa muda mrefu (miaka miwili) na hawana mpango wa kumuuza na ataendelea kusalia ndani ya kikosi cha Singida hadi hapo mkataba wake utakapofikia tamati.

Mirambo alisema wanapambana timu yao kufanya vizuri na kumaliza ligi katika nafasi ya tatu pamoja na kuhakikisha wanacheza fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC).

Singida Big Stars wako nafasi ya tatu kwennye msimamo wa Loigi Kuu Bara wakiwa na pointi 51, juu ya Azam FC ambao wako nafasi ya nne wakiwa na pointi 50, Simba nafasi ya pili alama 60 na Yanga ikiongoza msimamo kwa pointi 68 kabla ya mechi ya jana dhidi ya Simba.

Katika michuano ya ASFC, Singida Big Stars wametinga nusu fainali na watakutana na Yanga kwenye mchezo utakaopigwa Uwanja Liti mkoani, Singida nusu fainali nyingine ikiwakutanisha Simba na Azam FC katika Dimba la Nangwanda Sijaona lililopo Mtwara.

**BONASI...**




Mshindi wa Jackpot Bonus, Peter Maduhu, kutoka Moshi akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 6 baada ya kubashiri mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga si kwa Simba aisee*

INATOKA UKURASA 24

wango cha hali ya juu.

Hata hivyo, matokeo hayo hayajaathiri msimamo wa ligi, Yanga ikiendelea kukaa kileleni kwa pointi 68, Simba ikifuatia na pointi zake 63, lakini ikiwa imepunguza pengo kutoka pointi nane mpaka tano.

Katika hatua nyingine, kipa Ally Salim amezawadiwa kiasi cha Sh. milioni 10 baada ya ahadi hiyo kutolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again'.

Ahadi hiyo aliitoa juzi usiku katika kikao cha watu watano akiwamo, mwenyekiti huyo, wajumbe wawili na makipa wawili wa Simba, Salim na Beno Kakolanya aliyekuwa benchi katika mchezo huo wa jana.

Wakati huo huo, Rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed 'Mo' Dewji ameitisha kikao cha dharura cha wachezaji wake kuelekea katika mchezo wao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi wiki hii.

"Bosi alifanya mazungumzo na bodi na kutoa maagizo ya kutaka kukutana na wachezaji wake kuongea nao kuelekea mechi ya kimataifa, lengo ni kushinda hiyo mechi," alisema mtoa habari wetu.

Michezo

Jumatatu Aprili 17, 2023

Nipashe



Haaland azidi kuweka rekodi EPL UKURASA 21

SEMENI TENA...



Kulia ni beki wa kati wa Simba, Henock Inonga, akiifungia timu yake bao la kwanza kwa kichwa na kushoto ni kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Denis Kibu, akiachia bonge la shuti na kufunga bao la pili wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga si kwa Simba aisee

## ●●● Kipa Ally Salim ajazwa mamilioni, Inonga, Kibu waipiga mabao ya mwaka, Robertinho akiandika rekodi...

**Adam Fungamwango na**

**Saada Akida**

MABAO mawili yaliyofungwa na beki raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Henock Inonga na Mtanzania Denis Kibu, yalitosha kuiwezesha Simba kuibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga kwenye mechi kali ya 'dabi' ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana.

**Simba imeshinda mechi yake ya Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu Februari 16, 2019 ilipopata ushindi wa bao 1-0 lililowekwa wavuni na Meddie Kagere. Baada ya hapo zimepita mechi saba za Ligi Kuu, Yanga ikishinda mbili na sare tano.**

Na kwa mara ya kwanza msimu huu, Yanga imeshindwa kupata bao kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira na Msaidizi wake, Juma Mgunda wanashinda 'dabi' ya kwanza, lakini ikiwa si mara ya kwanza kwa Robertinho kuifunga Yanga.

Mara ya kwanza ilikuwa ni Agosti 29, mwaka 2018 kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika hatua ya makundi wakati akiifundisha Rayon Sports ya Rwanda, ikishinda bao 1-0 jijini Kigali, baada ya suluhu ya bila kufungana Mei 16, mwaka huo Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mara ya pili ni Agosti 6, mwaka jana wakati kocha huyo raia wa Brazil akiifundisha Vipers SC ya Uganda, alipoipa Yanga kichapo cha mabao 2-0, kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyopewa jina la Siku ya Mwananchi.

Katika mechi ya jana, ilianza kwa kasi na dakika ya pili tu ya mchezo, Simba iliandika bao la kwanza lililowekwa wavuni na beki wake wa kati Henock Inonga kwa kichwa, baada ya kuunganisha krosi iliyopigwa na Shomari Kapombe.

Beki huyo wa kulia alipokea pasi fupi ya mpira wa kona iliyopigwa na Clatous Chama, kabla ya kumiminina majalo hayo yaliyomkuta mfungaji.

Jean Baleke alikosa bao la wazi dakika ya 12, aliposhindana ubavu na mabeki wa Yanga, kabla ya kuwazidi lakini shuti lake lilikwenda nje akiwa anatazamana na kipa Djigui Diarra.

Fiston Mayele nusura aukwamishe mpira wavuni dakika moja baada ya Baleke kufanya shambulizi, alipoambaa na mpira katikati ya uwanja, na mita zipatazo 30 aliachia kombora ambalo lilidunda, lakini kipa Ally Salim alikaa imara akaupangua na kuwa kona.

Baada ya mabao hayo mawili Simba ilionekana kama kuridhika na kucheza nyuma wakiwaacha Yanga wakishambulia mfululizo.

Hata hivyo, walijisahau na kupeleka shambulizi la kushtukiza, ambapo nusura Simba ipate bao dakika ya 29 kama si Beleke kugongesha nguzo alipounganisha krosi ya Saido Ntibazonkiza.

Dakika mbili baadaye Simba ilipata bao la pili lililotiwa ndani ya kamba na Kibu Denis kwa shuti kali la juu lililomshinda kipa Diarra na kujaa wavuni.

Mpira huo ulianzia kwa wachezaji wa Yanga wenyewe ambao walipigiana pasi wakaupoteza katikati ya uwanja, Kibu akauchukua na kuondoka nao, ikionekana kama anaweza kumpasia Saido, lakini hakufanya hivyo, kwani kiasi cha mita 30 aliachia fataki liliotua wavuni.

Mayele alifanya majaribio mawili dakika ya 34 alipopiga shuti kali la mbali ambalo lilitemwa na kipa Salim kabla ya kuuwahi tena, na dakika nne baadaye aliwakosa Simba kwa kupiga nje, kutokana na uzembe na Mohamed Hussein kushindwa kuufagia mpira maeneo ya hatari.

Dakika moja kabla ya mapumziko, Baleke alikosa tena bao la wazi alipobaki yeye na Diarra kwa kupiga nje kidogo ya lango, baada ya pande safi kutoka kwa Chama.

Kipindi cha pili Yanga ilifanya mabadiliko ambapo waliwatoa Salum Aboubakar 'Sure Boy', Yannic Bangala na Jesus Moloko, wakiwaingiza Stephane Aziz Ki, Mudathir Yahaya na Tuisila Kisinda, ambayo yaliwasaidia sana kukamata eneo la katikati na kusukuma mashambulizi makali langoni mwa Simba.

Haikushangaza kuona dakika mbili baadaye Aziz Ki alipopiga shuti kali lililopaa langoni mwa Simba.

Simba ilimtoa Nyoni na nafasi yake ikachukuliwa na Nassor Kapama kusaidia kati kutokana na kutawaliwa zaidi na Yanga kipindi cha pili.

Kipa namba tatu wa Simba ambaye alilazimika kudaka mechi ya jana kutokana na Aishi Manula kuwa majeruhi, Salim alifanya kazi ya ziada kuokoa shuti la karibu la Tuisila Kisinda, ambapo lilimtoka na mpira ukamkuta Bernard Morrison ambaye naye aliingia kipindi cha pili, lakini alijitupa mzima mzima ili kuuzuia mpira huo usijae wavuni.

Salim alikuwa kikwazo kwa wachezaji wa Yanga pale walipopata nafasi chache za kushambulia, hivyo kuibuka shujaa wa mechi.

Kocha Mgunda alisema walimuandaa kipa huyo tangu mechi ya robo fainali ya Ihefu, ambayo nayo alicheza kwa ki-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >